SUPA JACKPOT
TZS. 1,151,104,636
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA
**Nyaraka** halisi ya siri ya polisi yapokewa kortini
UKURASA 5



UKURASA 11

# Nipashe

Jumamosi Septemba 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581428
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# Lissu akaidi amri Polisi

• **Atinga** Ngorongoro licha ya kupigwa 'stop', apokewa kwa... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**MCHENGERWA ATUMA SALAMU WAKURUGENZI WASIOTIMIZA WAJIBU**
WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)...

UKURASA WA 3
**PM AWAPA MAAGIZO MA-RC KUWABANA WADOKOZI**
WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maelekezo mahsusi manane yakiwamo...

UKURASA WA 4
**WAZIRI AWATOA HOFU WANANCHI UHABA DOLA**
SERIKALI imesema hali ya upatikanaji wa Dola nchini imeendelea kuwa himilivu...

## Mkulima ajiua kwa bastola shambani

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhi Tuzo ya Chakula Afrika 2023 kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Pan-Africa Bean Research Alliance (PABRA) ambaye pia ni Mkuu wa Mradi wa Maharage, Dk. Jean Claude Rubyogo, kwa niaba ya Taasisi hiyo ya Kenya, wakati wa hafla ya chakula cha jioni alichowaandalia viongozi na washiriki wa Mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), Ikulu, Dar es Salaam juzi. Katikati ni Rais mstaafu na Mwenyekiti wa Tuzo cha Chakula Afrika, Dk. Jakaya Kikwete. **PICHA: IKULU**

MKUTANO MIFUMO YA CHAKULA

# Mawaziri wataka kulegezwa masharti misaada kifedha

UK. 2

**MICHEZO** **STARS WALAMBA MIL.500 ZA RAIS SAMIA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Tundu Lissu akaidi amri ya polisi, atinga Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu,**
NGORONGORO

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amekaidi agizo la polisi la kutoingia Ngorongoro na kupata mapokezi kutoka kwa wananchi wa eneo hilo.

Lissu aliingia jana akiwa na msafara wake na kupokewa na wananchi, ambao ni wafugaji wa jamii ya Kimasai, wanaotakiwa kuhama kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) iliyoko mkoani Arusha.

Mapokezi hayo yalifanyika katika kijiji cha Ololosokwani kilichoko ndani ya eneo la Ngorongoro kwa ajili ya kuzungumza na wananchi wanaoishi na kufuga ndani ya hifadhi hiyo.

Wakati anaingia Ngorongoro, tayari kulikuwa na zuio la Jeshi la Polisi la kumtaka kusitisha mikutano yake ya leo na jana.

Kwa mujibu wa barua ya Septemba 6,mwaka huu, Polisi wilayani Ngorongoro kwenda kwa CHADEMA, mikutano yote iliyopangwa kufanyika katika kata tatu zilizoko Tarafa ya Loliondo na kata tatu Tarafa ya Ngorongoro ilizuiwa.

Katika ukurasa wake wa Twitter juzi, Lissu aliweka barua ya jeshi hilo ya kumtaka kusitisha mikutano hiyo, huku akisema ratiba ya kufanya mikutano katika eneo hilo iko pale pale.

"Polisi wamekataza mikutano ya hadhara Ngorongoro. Juzi serikali ya Rais Samia imekataza wabunge wa Ulaya kutembelea eneo hilo. Wanaficha kitu gani, licha ya jitihada za serikali? Sisi tutakuwa Ngorongoro kesho (jana)," aliandika Lissu kuhusiana na katazo hilo katika barua iliyotiwa saini na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Ngorongoro, Peter Lusesa.

Sehemu ya barua hiyo ilisomeka: "Yahusu kusitisha mikutano tarehe 08/09/2023 na 09//09 2023. Rejea somo tajwa hapo juu, pia yako KUMB: Na CDM/NGOR/V.1/01 ya tarehe 04/09/2023.

"Tunapenda kukufahamisha kuwa barua yako tajwa tumeipokea ikiwa na maudhui kufanya vikao vya ndani na mikutano ya hadhara maeneo ya kata tatu zilizoko tarafa ya Loliondo na kata tatu zilizopo Tarafa ya Ngorongoro.

"Hata hivyo, Tarafa ya Ngorongoro ni eneo la Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro na kwamba kuingia na kutoka eneo hilo ni sharti kufuata taratibu zinazosimamia eneo hilo (kupata kibali kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro). Aidha, kwa upande wa Tarafa ya Loliondo, kulingana na taarifa mbalimbali tulizo nazo, haziruhusu kufanya shughuli za kisiasa hasa mikutano ya hadhara.

"Kutokana na sababu hizo hapo juu, tunaelekeza kwamba usitishe mikutano hiyo kwa sasa hadi wakati mwingine ambao utakuwa mwafaka kwa ustawi wa amani na utulivu wa wilaya yetu. Tunatanguliza shukrani kwa ushirikiano wako na nawasilisha kwa hatua zako."



Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko, akizungumza wakati akifunga Mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Chakula Afrika (AGRF), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mchengerwa atuma salamu wakurugenzi wasiotimiza wajibu

**Na James Mwanamyoto,**
TAMISEMI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amesema mkurugenzi wa halmashauri atakayeshindwa kutekeleza ujenzi wa miradi ya afya atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mchengerwa aliyasema hayo jana wakati wa kikao kazi na watumishi wa idara ya afya, ustawi wa jamii na lishe wa TAMISEMI kilicholenga kujadili utekelezaji wa majukumu na kuhimiza uwajibikaji.

Alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI kuwataka wakurugenzi wote wa halmashauri kujipanga kikamilifu kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati.

Alisema kama kuna halmashauri imepelekewa fedha na kushindwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya afya, mkurugenzi atasimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi.

"Nipatieni orodha ya wote walioshindwa kukamilisha miradi, wabadhirifu wa fedha za miradi, waliojenga chini ya kiwango na wale ambao wamepelekewa fedha lakini bado ziko kwenye akaunti ili wachukuliwe hatua bila kuchelewa," alisema.

Mchengerwa aliwahimiza watendaji wanaosimamia ujenzi wa miradi hiyo, kufanya kazi kwa bidii na weledi kwa kuwa hahofii kuchukiwa na wale watakaoshindwa kutekeleza wajibu wao.

Pia aliwataka watendaji TAMISEMI kushirikiana na wawakilishi wa wananchi kubaini maeneo ya kujenga miundombinu ya afya kulingana na uhitaji.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alimwahidi Waziri kuwa idara hiyo haitamwangusha katika kutekeleza majukumu na maelekezo yote aliyoyatoa.

# Mawaziri wataka kulegezwa masharti misaada ya kifedha

**Na Waandishi Wetu**

MAWAZIRI wa Kilimo Afrika, wametoa rai kwa washirika wa maendeleo kurekebisha mifumo ya fedha, ili Afrika inufaike na rasilimali zake na zilizoko duniani.

Aidha, Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, amewataka viongozi wa serikali na sekta zinazohusika kwenye mnyororo wa mifumo ya chakula, kusimamia vizuri maazimio yaliyotolewa ili kuleta mageuzi yanayokusudiwa kwenye kilimo, mifugo na uvuvi.

Akizungumza kwa niaba ya mawaziri wenzake wakati wa kufunga mkutano wa 13 wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema Tanzania iko tayari kushirikiana na Mtandao wa Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA) kuandaa kikao cha mawaziri wa sekta hiyo ili kuweka vipaumbele vya kutekeleza maazimio yanayotokana na mkutano huo.

Alisema nia ni kuweka mpango wa maeneo ya kuelekeza fedha za wafadhili wa kilimo na mifumo ya chakula ili matokeo ya AGRF yaonekane.

"Tanzania tulikubaliana kutafuta fedha kwa ajili ya mifumo ya chakula. Tunawashukuru wote waliotoa ahadi ya fedha," alisema.

Alitaja washirika walioahidi fedha za kuboresha kilimo na kiasi kwenye mabano kuwa ni Benki ya Dunia (Dola za Marekani milioni 300), Benki ya Maendeleo Afrika (AFDB) (Dola milioni 100), AGRA (Dola milioni 40), benki ya CRDB (Dola milioni 50) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Misaada ya Kiufundi na Maendeleo ya Kilimo (IFAD) Dola milioni 60.

Alisema wadau wengine wameahidi Dola milioni tatu kwa ajili ya kuandaa mpango wa mageuzi ya kilimo wa mwaka 2050.

"Ujumbe wangu na wenzangu wa kilimo na mifugo, tunaiambia dunia asilimia 65 ya rasilimali ambazo hazijatumika ziko Afrika, tunataka dunia ijadili ni namna gani mitaji rahisi inapatikana duniani. Afrika haihitaji kusaidiwa, inahitaji kupewa haki yake kwenye keki ya dunia ili kutumia rasilimali kujiletea maendeleo," alisema.

Awali, akifunga mkutano huo kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Biteko alisema mkutano huo umetoa njia ya kuimaisha mifumo ya chakula na kwamba ni wajibu wa viongozi wa ngazi zote kuhakikisha hilo linatimia. Alisema mijadala yote iliyozungumzwa na kutoa maazimio, yatawasilishwa serikalini kwa ajili ya utekelezaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa AGRF, Amath Pathe Sene, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna Tanzania ilivyoandaa mkutano huo. Alisema mkutano umehudhiriwa na watu 5,400 kutoka nchi 90 duniani, idadi ambayo alisema ni kubwa kuliko ilivyotarajiwa.

Alisema miongoni mwao kulikuwa na wakuu watano wa nchi, marais sita wastaafu, mawaziri wa kilimo, afya, biashara na mifugo zaidi ya 30, wakurugenzi 1,200 kutoka sekta binafsi na mashirika manane makubwa ya kimataifa yanayohusika na mifumo ya chakula.

Alizipongeza kampuni za Tanzania zilizodhamini mkutano huo huku akibainisha kuwa mwakani AGRF itafanyika Rwanda.

**Imeandikwa na Restuta James, Jenifer Gilla na Renatha Msungu.**

HABARI KITAIFA

# Mkulima ajitwanga risasi shambani kwake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKULIMA maarufu wa tumbaku na mkazi wa Kitongoji cha Namba Tisa "A", kijiji cha Ilomelo, Ushetu mkoani Shinyanga, Safari Manjala, amejiua kwa kujipiga risasi kwa kutumia bastola yake.

Tukio hilo lilitokea jana, majira ya saa 2:00 asubuhi katika kitongoji cha Namba Tisa "A" akiwa kwenye shamba lake la miti huku sababu za kutekeleza tukio hilo zikiwa hazijafamika mpaka sasa.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kennedy Mgani, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema Manjala alijipiga risasi chini ya kidevu na sikio la kulia. Alisema chanzo bado hakijafahamika na wamеuchukua mwili kwa uchunguzi zaidi.

Alisema jeshi hilo linaendelea na upelelezi kwa kuwahoji ndugu, jamaa na marafiki ili kubaini chanzo cha tukio hilo na utakapokamilika watakabidhi mwili kwa ndugu ili kuendelea na taratibu za mazishi.

Diwani wa Kata ya Ulowa, Gabriela Kimaro, alisema tukio hilo limewashangaza kutokana na uamuzi aliochukua mkulima huyo maarufu kwa kuwa wamezoea kusikia watu wanajinyonga kwa kamba na kuacha ujumbe mbalimbali lakini amejiua kwa kujipiga risasi bila kuacha ujumbe wowote.

Alisema licha ya kuwa mkulima mkubwa na kuiingizia mapato Halmashauri ya Ushetu, pia alikuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Ulowa.

Kimaro alisema kabla ya kuchukua uamuzi huo, Manjala aliamka akiwa mzima na alionekana shambani kwake kama mtu anayekagua shamba lake lakini baadaye ulisikika mlio wa risasi na baadaye kubainika kuwa amefariki dunia kwa kujiua.

"Sisi sote hapa hatufahamu sababu iliyomfanya kujipiga risasi shambani kwake tena kwa kujipiga risasi kwenye koo hadi risasi kutokeza kichwani. Tunasubiria taarifa ya Polisi baada ya kumaliza upelelezi, hivyo niwaombe wananchi watulie," alisema Kimaro.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo, alisema Manjala alikuwa mmoja wa wakulima wanaochangia mapato ya ndani ya halmashauri kutokana na mamlaka hiyo ya serikali za mitaa kutegemea mapato kupitia zao hilo.

Alisema watu wanapopata msongo wa mawazo waache kuchukua sheria mkononi badala yake watafute ushauri kwa watu wa karibu yao.

Mihayo alisema siku kadhaa zilizopita walishiriki naye katika mkutano mkubwa uliofanyika Kata ya Ulewe uliokuwa umeitishwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, na wameshangaa kupata taarifa kuwa amejipiga risasi shambani.

Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Kahama, Hassan Haruna, alisema chama kimepokea msiba huo kwa masikitiko na taarifa za kifo hicho alizipata kwa wanajumuiya walioko Ulowa na sababu za kifo hicho bado hazijafahamika.

# Majaliwa aagiza Ma-RC kuwabana watumishi wadokozi halmashauri

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maelekezo mahsusi manane yakiwamo kwa Wakuu wa Mikoa kufuatilia watumishi wabadhirifu wanaosababisha upotevu wa mapato ya serikali na kuwachukulia hatua mara moja.

Ametaka hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya watumishi wote wanaosababisha upotevu wa mapato ya serikali na kwa wakuu wa mikoa wahakikishe wanatoa taarifa kwa mamlaka.

Maelekezo mengine amewataka watumishi wa umma watenge muda wa kwenda kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika maeneo yao.

Majaliwa aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa wakati wa kuahirisha Mkutano wa 12 wa Bunge uliofanyika kwa wiki mbili kuanzia Septemba 29, mwaka huu.

"Wafuateni, wasikilizeni na kutatua kero zao ili wasipoteze muda mwingi kufuatilia lakini pia wasilazimike kwenda ngazi za juu au kusubiri ziara za viongozi wa kitaifa kwa masuala ambayo mngeweza kuyafanyia kazi," aagiza.

Majaliwa amewataka waajiri wachukue hatua za kuimarisha mifumo ya kuwalinda wafanyakazi wao dhidi ya vihatarishi vilivyomo katika maeneo yao ya kazi.

"Hatua hizo ni pamoja na kuwa na mwongozo wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, kufanya tathmini ya vihatarishi mahali pa kazi, kuhakikisha wafanyakazi wao wanapimwa afya ili kubaini athari ya vihatarishi kwa mfanyakazi na kuhakikisha maeneo yao yanafanyiwa kaguzi za usalama na afya ili kuwalinda wafanyakazi na kulinda uwekezaji wao.

"Nitoe wito kwa watumishi wa OSHA (Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi) wawe waadilifu wanapoendesha ukaguzi mahali pa kazi na kuchukua vipimo vya wafanyakazi," alisema.

Pia aliwataka wafanyakazi wahakikishe wanazingatia taratibu na miongozo ya kujilinda dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kusababisha ajali au magonjwa wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao.

Alisema hiyo itasaidia kulinda afya na usalama wao pamoja na kumpunguzia mwajiri gharama za uendeshaji pale wanapougua au kupata ajali wakiwa kazini.

Kadhalika, alitaka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) uongeze wigo wa kutoa elimu kwa wafanyakazi ili watambue huduma zinazotolewa na mfuko huo.

Vilevile, alisema waajiri watumie ipasavyo mifumo ya TEHAMA kupata huduma, kujisajili na kuwasilisha kwa wakati michango katika mfuko huo.

"Nipende kuwasisitiza wafanyabiashara na watoa huduma watoe risiti halali kupitia mashine za kielektroniki (EFD) wakati wa mauziano ya bidhaa au utoaji wa huduma kwa wateja. Kwa upande wa wateja, niwakumbushe kuwa ni wajibu wao kudai risiti yenye thamani halisi ya fedha walizotoa," alisema.

Pia aliwataka maofisa masuuli waimarishe usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na kutekeleza kikamilifu Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 na watendaji wa serikali, waimarishe ukusanyaji wa mapato na kufanya matumizi kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa katika bajeti sambamba na kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Aliwataka pia waweke utaratibu wa kufanya ukaguzi mashine za 'POS' ili kubaini kama kuna ukiukwaji wowote unaofanyika sambamba na kuwa na utaratibu endelevu wa ufuatiliaji na mfumo wa usalama maalum wa utunzaji taarifa (back-up).

"Niwakumbushe watumishi wa umma kuwa bado tunalo jukumu la kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato kama Rais Samia Suluhu Hassan, alivyosisitiza kuhusu usimamizi wa ukusanyaji mapato kwenye mamlaka za serikali za mitaa wakati akifunga mafunzo ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa mjini Kibaha," alisema.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

## MNADA WA HADHARA WA BOTI CHAKAVU

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwatangazia Umma kuwa inatarajia kufanya mnada wa hadhara wa **Boti chakavu mbili (02)** pamoja na **Rubber Boti 2** ambazo zipo Zanzibar na Dar es salaam. Mnada huo utafanyika kwa njia ya mtandao mnamo tarehe **25 Septemba, 2023.**

Boti moja (01) imeegeshwa katika ofisi za **Bandari – Zanzibar** na boti moja (01) imeegeshwa katika **Kamandi ya Jeshi la Maji (Navy Kamandi – Kigamboni) Dar es Salaam.** Aidha, Rubber Boti mbili (02) zipo katika **Maegesho ya Kontena Bandari ya Dar es Salaam**

Wananchi wataopenda kushiriki mnada wataweza kuona boti hizo kupitia tovutu ya **https://www.tra.go.tz** kuanzia tarehe 11/09/2023 au wafike katika ofisi za TRA za Zanzibar na Dar es Salaam (Ofisi za Forodha na Ushuru wa Bidhaa Makao Makuu) kwa ajili ya ukaguzi kabla ya kushiriki mnada huo.

Masharti ya Mnada kwa washiriki ni kama ifuatayo;

1. Mnada huu ni kwa wananchi wote,
2. Kila Mwananchi ana haki ya kushiriki katika mnada,
3. Bidhaa itauzwa kama ilivyo mahali ilipo,
4. Malipo yote ni ya fedha taslimu ambapo malipo ya awali ya kiwango cha 25% yatatakiwa kulipwa ndani ya masaa (24) kulingana na taratibu za uendeshaji wa minada. Kiwango cha 75% kilichobaki kitalipwa ndani masaa 48. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi na malipo ya awali yaliyolipwa hayatarudishwa,
5. Mnunuzi atalazimika kulipia asilia (100%) ya thamani yote na kuondoa kifaa/vifaa atakavyonunua,
6. Ruhusa ya kuangalia vifaa imetolewa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe 11/09/2023 hadi tarehe 25/09/2023 katika ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania zenye bidhaa kama taarifa za bidhaa husika zilivyoainishwa mnadani,
7. Mnada utaanza siku ya tarehe 25/09/2023 saa sita na dakika moja (6:01) usiku na kuisha siku ya tarehe 25/09/2023 saa tano kamilil (5.00) asubuhi,
8. Vigezo na masharti kuzingatiwa.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **Tovuti** | : | **www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | : | **0800 750 075 / 0800 780 078 au 0800110016** |
| **WhatsApp** | : | **0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | : | **huduma@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu".***

**Imetolewa na**
**IDARA YA ELIMU KWA MLIPAKODI NA MAWASILIANO**

# Waziri awatoa hofu wananchi uhaba Dola

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema hali ya upatikanaji wa Dola nchini imeendelea kuwa himilivu na akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,246.7 kwa Julai, mwaka huu.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Biharamulo Magharibi (CCM), Ezra Chiwelesa.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali katika kunusuru uchumi wa nchi kutokana na ukosefu wa fedha za kigeni, hususani Dola ya Marekani.

Akijibu swali hilo, Dk. Nchemba alisema pamoja na vikwazo vilivyopo, upatikanaji wa fedha za kigeni nchini ni himilivu na kiasi kilichopo kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takriban miezi 4.7 ikilinganishwa na malengo ya miezi minne.

Serikali, alisema inaendeleea kuchukua hatua mbalimbali za muda mfupi wa kati na muda mrefu katika kukabiliana na vikwazo ya upatikanaji wa fedha za kigeni, hususani Dola ya Marekani.

"Vikwazo hivyo vimesababishwa na athari za vita kati ya Ukraine na Russia, kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii baada ya UVIKO-19 na mabadiliko ya tabianchi.

"Sababu nyingine ni utekelezaji wa sera za fedha ambayo inalenga kupunguza ukwasi katika uchumi wa nchi mbalimbali ikiwamo Marekani ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei. Kwa ujumla, matukio hayo yameathiri mnyororo wa uzalishaji, usambazaji na uhitaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia," alisema.

Alitaja hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali kupunguza athari za upatikanaji huo ni pamoja na kuongeza kiwango cha kuuza fedha za kigeni katika soko la fedha za kigeni. kati ya Machi, 2022 na Agosti, mwaka huu, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeuza katika soko la fedha za kigeni zaidi ya dola za Marekani milioni 500.

Pia alisema jitihada zingine ni kuongeza vyanzo vya upatikanaji wa fedha za kigeni ikiwemo ununuzi wa dhahabu, kutekeleza mikakati ya kuongeza mauzo nchi za nje na kuzalisha bidhaa mbadala wa zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Kadhalika, alisema serikali imepanga kuendelea kushirikisha benki za biashara, maduka ya kubadilisha fedha za kigeni pamoja na wadau wengine katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya usimamizi wa fedha za kigeni nchini.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kunusuru wakandarasi ambao wameathiriwa na upungufu huo wa Dola na mkakati wa serikali wa kuhakikisha hauathiri utekelezaji wa bajeti.

Akijibu swali hilo, Waziri Nchemba alisema serikali imechukua hatua ya kuhakikisha inabana matumizi ili kutoa fursa miradi ya wananchi isiathiriwe.

## Mbunge alia nauli kubwa ATCL

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Asha Abdullah Juma, ameiomba serikali kufanya mapitio ya bei ya nauli za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alihoji kwa nini serikali haifanyi utafiti wa bei za safari za ndege ndani ya nchi kutokana na bei hizo kuwa kubwa.

"Kwa mfano Dodoma hadi Dar es Salaam bei ni kuanzia Sh.250,000 hadi Sh. 500,000 kwa safari ya mara moja. Serikali haioni hatari ya kupoteza soko la ndani endapo yakajitokeza mashirika mengine? Kuna shirika linafanya safari hiyo ya kwenda na kurudi kwa Sh. 450,000. Kwa nini msiokoe ATCL isije kuzama?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema kwa kawaida nauli za safari za ndege hupangwana soko kulingana na aina ya huduma inayotolewa.

"ATCL kama ilivyo kwa mashirika mengine ya ndege yanayotoa huduma zake kibiashara, nauli zake zinapangwa na soko kwa kuzingatia matakwa ya sheria za ushindani. Vigezo vinavyotumika katika kupanga nauli hizo ni pamoja na gharama za uendeshaji ili kuhakikisha mashirika ya ndege yanahimili ushindani wa soko na kujiendesha kwa tija na ufanisi," alisema.

"Utafiti umekuwa ukifanyika na watafanya zaidi. Kwa sasa ATCL haijapoteza soko na viwango vilivyowekwa ni kwa mujibu wa ushindani,"alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo, alihoji mpango wa serikali wa kuhakikisha zinapatikana ndege za moja kwa moja za Dodoma kwenda Kilimanjaro na Arusha au muda mfupi wa kuunganisha kupitia Dar es salaam.

Akijibu swali hilo, Kihenzile alisema serikali imepokea ushauri huo na itafanyia kazi.

**Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alihoji kwa nini serikali haifanyi utafiti wa bei za safari za ndege ndani ya nchi kutokana na bei hizo kuwa kubwa.**



Diwani wa Viti Maalum wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Fatuma Kingwande akichangia maoni katika kikao cha wadau wa maendeleo wa mkoa huo na Dar es Salaam, kilichofanyika Mbagala juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Profesa UDSM atoa mbinu ufaulu shuleni

**Na Mwandishi Wetu**

MWANATAALUMA mbobezi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Goodluck Urassa, amesema ili shule zifanye vizuri kitaaluma, walimu wanapaswa kufanya kazi kama sehemu ya biashara na kuongeza ubunifu.

Prof. Urassa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akiwajengea uwezo walimu wa shule za Kimataifa za St. Mary's, ili kuongeza ubunifu na ufanisi katika ufanyaji kazi wao.

Alisema lengo la semina hiyo ni kuwapiga msasa walimu hao katika mambo mengi ikiwamo elimu ya ujasiriamali, ubunifu na namna ya kuongeza ufaulu katika shule zao kwa ajili ya kuzikuza kitaifa.

"Nimewapiga msasa namna ya kufanya kazi kwa viwango vya juu, jinsi ya kuhudumia wateja, kuendesha shule zao kibiashara na kijasiriamali" alisema.

Pia aliwataka walimu kujenga utamaduni wa kuwa na mpango wa kufanya kazi kuanzia mwanzo wa mwaka hadi mwisho wa mwaka pamoja na ule wa kila siku katika kutimiza majukumu yao ya kitaaluma.

"Shule nyingi, zinaathirika kwa kutojenga vizuri mipango yao, na kukosa rasilimiali za kujiendesha ndiyo maana tunawajengea walimu na viongozi uwezo ili wakawarithishe na wanafunzi wao ili tuje kupata viongozi bora wa baadaye," alisema.

Pia alizisihi taasisi za elimu kukumbuka umuhimu wa kutoa semina kwa watumishi wa serikali, ili waweze kukumbuka majukumu yao, muhimu wa kazi yao na kuongeza ufanisi katika kazi akisema kuwa njia hiyo itasaidia kupata matokeo chanya kwenye sekta.

Mkurugenzi wa Shule za St. Mary's Tanzania, Dk. Rose Rwakatale, alisema lengo la semina hiyo ilikuwa kuwainua wafanyakazi wao, na kuwaongeza elimu ili waweze kutimiza majukumu yao kulingana na mabadiliko ya teknolojia.

Alisema semina hiyo iliwakutanisha walimu kutoka shule 14 zilizoko Dar es Salaam na mikoa mingine kwa lengo la kusikiliza, kuchambua kwa kina na hatimaye kwenda kufanyia kazi ili kuongeza ufanisi kwenye shule zao.

Mkuu wa Shule ya St Mary's Tabata, Thomas Samson, alisifu semina hiyo akisema imewafungua kwa kiasi kikubwa kwani wamefundishwa namna ya kuwahudumia wateja, majukumu ya viongozi katika taasisi.

"Baada ya semina hii matokeo yatakuwa makubwa, tumefundishwa vitu vingi, tumeongeza maarifa na ujuzi, imekuwa siku nzuri kwetu kujifunza kutoka kwa Profesa mbobezi tunategemea kuhamishia maarifa haya kwenye maeneo yetu ya kazi," alisema.

Aliushukuru uongozi wa shule hizo kwa kuandaa semina hiyo, aliyoita elimishi akiomba liwe jambo endelevu.

# Wamiliki malori watoa mapendekezo matano ya kumaliza uhaba wa mafuta

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TAMSTOA) kimetoa mapendekezo matano kwa serikali kumaliza uhaba wa mafuta ya dizeli na petroli unaoikumba nchi kila wakati.

Moja ya pendekezo ni serikali kuangalia upya utaratibu wa kuagiza mafuta kwa sababu kuna mazingira ya mchezo mchafu unaofanywa na baadhi ya wahusika.

Mwenyekiti wa chama hicho, Chuki Shabani, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya uhaba wa mafuta inayoendelea sasa nchini licha ya serikali kutoa maelekezo.

Pamoja na mambo mengine, Shabani alisema serikali inapaswa kuwa na akiba ya mafuta yake na kwamba pindi panapotokea uhaba, akiba hiyo itumike.

Pendekezo lingine alilitaja kuwa ni serikali iangalie upya utaratibu unaotumika kuuza mafuta, akisema ni jambo lisiloingia akilini kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inapokaribia kutangaza bei mpya, nishati hiyo inaanza kuadimika na inapotangazwa kupanda inapatikana.

Alisema pia serikali inaweza kuanzisha utaratibu wa kutafuta mafuta ya ruzuku kama Wizara ya Kilimo inavyofanya kwenye pembejeo.

Kwa mujibu wa Shabani, pendekezo lingine ni serikali kupiga marufuku sekta binafsi kuagiza mafuta na kwamba serikali ndiyo ibebe dhamana ya kuagiza nishati hiyo.

"Serikali ikifuata hayo, ninatumaini tutakuwa tumeondoka na tatizo hili kwa sababu haiwezekani kila mara hili tatizo lipo. Kwa mfano nchi moja, Tanzania Bara bei ni tofauti na Zanzibar. Kwa mfano Zambia bei ya mafuta iko chini wakati wao wanachukua mafuta Bandari ya Dar es Salaam," alisema Shabani.

Pia alisema hadi sasa baadhi ya maeneo mafuta ya dizeli na petroli yanapatikana kwa shida na sehemu zingine bei iko juu.

"Kilio hiki akisikie Waziri Mkuu, Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Nishati, bei ya mafuta inatuletea shida sisi katika usafirishaji. Hata wenzetu wa mabasi nao wanalalamika. Serikali iangalie matibabu ya suala la mafuta kwa sababu kila mtanzania linamgusa," alisema Shabani.

Pia alisema endapo serikali haitachukua hatua za haraka kumaliza tatizo hilo, kuna hatari ya bei ya bidhaa, usafirishaji ikaongezeka hali itakayowaumiza Watanzania wenye kipato kidogo.



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Alex Makulilo, akifungua mafunzo ya uhariri kwa wahariri wakuu wa majarida ya kitaaluma kwa chuo hicho, yaliyofanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere Kibaha, mkoani Pwani jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

KESI DADA BILIONEA MSUYA:

# Nyaraka halisi ya siri ya polisi yapokewa kortini

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imepokea nyaraka halisi ya siri ya Jeshi la Polisi ya tukio la awali la mauaji ya dada wa Bilionea Msuya, Aneth Msuya, ambayo ndiyo ilikuwa ikitumika mara kwa mara ndani ya jeshi hilo na si ile ambayo ililetwa na upande wa utetezi.

Katika kesi hiyo, Miriam Mrita ambaye ni mke wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya, na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wanadaiwa kuwa Mei 25, 2016 walimuuwa Aneth nyumbani kwake, Kibada, Kigamboni , Dar es Salaam.

Kielelezo hicho kilitolewa na Ofisa wa Polisi kutoka Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai mkoani Dodoma, Sajenti Obadia Mwarukuta na kupokewa mbele ya Jaji Edwin Kakolaki, wakati akitoa ushahidi wake.

Alidai kuwa mwaka 2016 alikuwa Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai mkoani Dar es Salaam Kitengo cha Kumbukumbu za Makosa ya Jinai na kwa sasa yuko Kitengo cha Kupambana na Dawa za Kulevya.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, Sajenti Mwarukuta alidai kuwa Mei 30, 2016 aliingia kazini na wakati anaendelea na kazi zake zingine alizopangiwa, kuna nyaraka alizipokea kutoka mkoa wa kipolisi wa Temeke zinazohusiana na jinai.

Alidai nyaraka hizo zingine zilikuwa za mauaji na anakumbuka zilikuwa taarifa tatu za awali za mauaji, moja ilikuwa mlinzi wa ghala kuuawa, vibaka watatu waliuawa na wananchi wenye hasira kali na ya tatu ilikuwa ya mauaji ya Aneth Msuya.

Sajenti Mwarukuta alidai kuwa baada ya kuzipokea aliziweka kwenye faili maalum la mauaji na faili hilo liko ofisini kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na kwamba yeye ndiye anatunza nyaraka hizo.

"Inaweza ikatokea DCI au ofisa yeyote anahitaji nyaraka hizo, nampelekea ofisini kwake. Akishazifanyia kazi naenda kuzichukua na kurudisha kwenye mafaili husika na pia nyaraka hii kwa baadaye inaambatanishwa na nyaraka za maendeleo ya kesi," alidai.

Mwarukuta alidai kuwa akiona FCR ya Aneth Msuya ataikumbuka kwa kupitia namba za kesi ya kituo cha polisi husika, namba ya kesi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa (RCO) na pia ataitambua kwa sababu yeye ndiyo aliipokea.

Shahidi huyo alipewa nyaraka na Wakili Kimweri ili kuitambua kama ndiyo aliyokuwa anaielezea na kudai kuwa ndiyo yenyewe na ilikuwa ilani ya kwanza ya tukio hilo.

"Mheshimiwa Jaji niko tayari nyaraka hii ipokelewe mahakamani kama kielelezo kwa sababu mimi ndiye nilipokea taarifa hiyo na kuitunza," aldai.

Baada ya ombi hilo, mawakili wa utetezi Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko, walidai kuwa hawana pingamizi na kielelezo hicho, hivyo mahakama ilikipokea kuwa kielelezo namba PE 17.

Wakili Kimweri aliiomba mahakama hiyo imruhusu shahidi asome nyaraka hiyo na pia aliiomba mahakama kupewa kielelezo DE (iii) ambacho ni nakala ya nyaraka ya FCR ambayo ni kielelezo cha upande wa utetezi ili alinganishe.

Jaji Kakolaki alimruhusu kusomwa kwa nyaraka hiyo na kupewa kielelezo DE (iii). Shahidi huyo alikisoma na kuchambua tofauti ambazo zipo kwenye vielelezo hivyo vya mahakama.

"Hizi nyaraka mbili nikizingalia DE (iii) ni nakala na hii PE 17 ni nyaraka halisi. Kwa uhalisia hazifanani. Nikiangalia eneo la juu ya hizi nyaraka kuna utofauti wa kwa jinsi zilivyojazwa," alidai.

Mwarukuta akiendelea kuongozwa na Wakili Kimweri, alidai kuwa kielelezo PE 17 kwenye namba ya upelelezi ya RCO mahali ilipoandikwa ni chini ya neno 'confidential' (siri), ndipo linapotakiwa iandikwe.

" Lakini kwenye hiki kielelezo DE III namba ya RCO imeandikwa sehemu iliyoandikwa to DCI 'copy' chini ya maneno ya FCR, ambapo iliyokuwa sahihi ni ya PE 17," alidai.

Pia alidai kuwa kielelezo PE 17 namba ya RCO ya jinai imeandikwa DSM/TMK/ CID/ SCR/2062/2016 na ya kielelezo DE III imeandikwa DSM/ Temeke/CID/SCR/2062/2016.

" Nataka kufafanua ukiangalia kwenye DE III neno Temeke limeandikwa lote, kwa mfumo wa kipolisi tunatumia maneno kwa ufupisho," alidai

Alidai kuwa ukiangalia mwisho wa nyaraka ya DE III sehemu iliyoandikwa hearing date imejazwa Julai 11,2016 na katika PE 17 hakuna kilichojazwa na hii fomu ya FCR inajazwa pindi tukio la jinai linapotokea.

"Ufafanuzi hii ilani ya kwanza inajazwa pale tukio la jinai linapotokea haiwezekani siku hiyo hiyo upelelezi bado unaendelea halafu ipewe tarehe ya kusikiliza kesi ni kitu ambacho haiwezekani," alidai.

Shahidi alidai kuwa kiuhalisia kielelezo PE 17 ndiyo kielelezo halisi cha Jeshi la Polisi ambacho ni siri inayotembea ndani ya jeshi hilo, sasa hii nyingine siijui," alisema

Kimweri: Kwenye kielelezo PE 17 sehemu ya mtuhumiwa kimejazwa nini?

Shahidi: Mtuhumiwa bado hajapatikana, lakini kwenye DE III imeandikwa mtuhumiwa ni Getruda Mfuru ambae ni dada wa kazi, ambapo katika eneo la kukamatwa kwenye nyaraka ya DE III imejazwa Yes na kwenye PE 17 imejazwa No.

Kimweri: Unapoiona hiyo nakala ya DE III, imezalishwa kwenye nakala halisi?

Shahidi: Hapana haijazalishwa huko.

Pia, alidai kuwa kwenye nyaraka hiyo inaonesha mtuhumiwa ni Getruda Mfuru ndiyo aliyehusika na mauaji, lakini katika maelezo yake imeandikwa kuwa watu wasio fahamika ndiyo wamefanya tukio hilo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Jumatatu saa 3:00. Shahidi namba 23 ataendelea kuulizwa maswali ya dodoso na wakili Kibatala.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Stars kufuzu AFCON, maandalizi yake yaanze sasa

**RAIS** Samia Suluhu Hassan ameendelea kuwa na mguu mzuri kwa timu za Tanzania kufanya vyema katika mashindano mbalimbali ya kimataifa wanayoshiriki.

Mwaka jana, tulishuhudia Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Girls, ikikata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia (U-17), tena ikiwa na Kocha Mkuu Mzalendo, Bakari Shime.

Lakini pia chini ya Rais Samia, klabu ya kutoka Tanzania, Yanga ilifanikiwa kucheza fainali za mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ikiwa imepita zaidi ya miaka 20, taifa likiwa halijafikia hatua hiyo.

Na juzi kwa mara nyingine, Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ilikata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), michuano hiyo itachezwa kuanzia Januari, mwakani huko Ivory Coast.

Taifa Stars imepata tiketi hiyo baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi F ikiwa na pointi nane nyuma ya vinara, Algeria waliofikisha pointi 16, ni baada ya kuwalazimisha Waarabu hao sare ya bila kufungana.

Hii ni mara ya tatu kwa Taifa Stars kufuzu fainali hizo, mara ya kwanza ilikuwa mwaka 1979 (fainali zilifanyika Nigeria) na mara ya pili ni mwaka 2019 ambapo michuano yake ilichezwa Misri.

Hongera za dhati zinatakiwa zianzie kwa serikali ya Rais Samia ambayo imeshiriki kwa namna mbalimbali hadi Taifa Stars imefikia malengo yake, ilishiriki kulipia baadhi ya gharama za kambi, safari, posho na mshahara wa benchi la ufundi la timu hiyo iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Adel Amrouche.

Lakini pia viongozi Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kufanikisha kumpata Amrouche na wasaidizi wake, kutosikiliza 'kelele' za wadau pale ambapo timu hiyo ilishindwa kupata matokeo chanya na kujifungia kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa kuendelea na safari hiyo ambayo juzi ilikamilika kwa furaha, nao wanastahili pongezi.

Mashabiki na wadau mbalimbali wa soka kwa kujitokeza kushangilia timu hiyo katika mechi zake za nyumbani na hata baadhi walijitahidi kusafiri kwenda ugenini kuwaunga mkono.

Baada ya pongezi, ikiwa imepita miaka minne tangu kushiriki fainali za mwaka 2019, huu ni wakati wa timu hiyo sasa kuanza maandalizi mapema ili iende kushindana na si kushiriki kama ilivyokuwa wakati mwingine.

Taifa Stars inahitaji kufanya maandalizi yake kwa kuzingatia mazingira halisi ya wachezaji wake kama inahitaji kupata matokeo chanya katika fainali hizo za AFCON kwa sababu inakwenda kukutana na timu zenye wachezaji wengi wakongwe na wazoefu.


Na ili kufikia malengo ya kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika fainali hizo, huu ni wakati wa TFF kukutana na klabu kupanga ratiba rafiki za mechi za Ligi Kuu pamoja na michuano ya Kombe la FA, zitakazosaidia wachezaji kupatikana pale Amrouche atakapowahitaji.

Ingawa zipo kanuni za FIFA kuhusu muda ambao wachezaji wanatakiwa kukutana kabla ya kwenda katika majukumu ya kimataifa, bado idadi kubwa ya wachezaji wa Tanzania wanacheza ligi ya ndani na kiuhalisia wanahitaji kuandaliwa na kujengwa zaidi tofauti na nchi nyingine ambazo vikosi vyao vinajumuisha nyota wengi wanaocheza Ulaya.

Kufanya vizuri kwa Stars, ni lazima tuwe tayari kama nchi kujitolea kwa kuweka mbele maslahi ya timu hiyo kama ambavyo tunazipa kipaumbele klabu zetu pendwa za Simba na Yanga, huu ni ukweli usiojificha.

Serikali, TFF na wadau wote, huu ndio wakati wa kushirikiana ili kuijenga Stars na tunaamini itafika kule ambapo mataifa mengine yaliyoendelea yamefika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Taifa Stars kufuzu AFCON bila ya kamati inawezekana

Na Adam Fungamwango

**BILA** kamati za hamasa wala za ushindi, timu ya soka ya Taifa (Taifa Stars), imefuzu kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazofanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwakani nchini Ivory Coast.

Miaka kadhaa nyuma ilionekana kama vile bila ya kamati za ushindi pamoja na hamasa, Stars haiwezi kufanya chochote kile.

Ni kamati zilizokuwa zikirundika watu wengi wakiwamo wanasiasa na wasanii ambao kazi yao ilikuwa ni kuhamasisha, kutoa fedha au kuhamasisha wengine kuiunga mkono timu hiyo.

Hawa walikuwa wakisafiri na timu nchi mbalimbali, lakini mara nyingi haikuonekana tija yoyote, badala yake walikuwa wakiitia timu presha.

Si kamati hizi ni mbaya, lakini ufanyaji kazi wao ulionekana kuwa wa kisiasa zaidi wengine kujipatia sifa binafsi na si kuisaidia Stars.

Binafsi naona tangu Rais, Samia Suluhu Hassan kutia mguu wake kwenye michezo, ikiwamo kuibeba Taifa Stars, huku akiwahamasisha wachezaji kwa kuahidi pesa ni kama kamati zimekufa kifo cha kawaida.

Huko nyuma, baadhi ya wachambuzi walikuwa wakishauri kuondokana na kamati hizo ambazo hazina umuhimu sana zaidi ya kuwapa presha tu wachezaji.

Kwa sasa Rais Samia anaahidi tu fedha, halafu kazi inaachwa kwa benchi la ufundi na wachezaji wake wanafanya kazi yao kimya kimya na mambo yanaenda.

Na uzoefu umeonyesha mara nyingi zinapoundwa Kamati za Ushindi na Uhamasishaji, Stars huwa haifanyi vizuri.

Na inaweza kufanya vyema katika mechi za mwanzo, lakini inapokuja mechi muhimu ambayo ni lazima ishinde ndipo zinapoundwa hizo kamati na Stars inaambulia patupu.

Nadhani hii imesababisha hata Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' kukumbuka yaliyotokea nyuma na kukubaliana na ushauri wa baadhi ya wadau kuachana na kamati.

> **Na uzoefu umeonyesha mara nyingi zinapoundwa Kamati za Ushindi na Uhamasishaji, Stars huwa haifanyi vizuri.**

"Hamasa haijafanyika kama zile zilizofanyika kipindi kilichopita kwa sababu tulishauriwa sana hapa katikati, miongoni mwa mambo tunayokosea ni kuipa presha kubwa timu yetu, lakini yale ambayo serikali inatakiwa kuyafanya ndani ili kuhakikisha timu inakuwa kwenye kiwango kinachoridhisha na wachezaji wapo katika hali nzuri yote tumeyafanya, huku ndani mpaka timu imesafiri na hata huko tunahakikisha ipo salama na huduma zote huku ikienda kwenye mchezo ikiwa katika nafasi ya kushinda," alisema Waziri huyo siku moja kabla ya mechi.

Tunampongeza yeye na Waziri, Dk. Damas Ndumbaro, kwa kusikiliza ushauri wa wadau wanaoitakia mema nchi ambao waliona kuna tatizo kukiundwa kamati mbalimbali.

Najua Kamati ya Ushindi ambayo kwa kiasi kikubwa inahusika na masuala ya kuwapa motisha wachezaji wamekufa kifo cha kawaida kwa Rais Samia mwenyewe kuamua kutoa fedha za motisha pale kila Stars inaposhinda, lakini ile ya hamasa haikuwapo kwa sababu ya Dk. Ndumbaro na 'Mwana FA' kuwa wasikivu.

Najua Rais Samia kama kawaida yake ataongeza 'mzigo' Stars itaelekea kucheza AFCON, lakini viongozi wa Wizara wanatakiwa kuendelea kuwa makini na kamati.

Timu imeshafuzu kuna watu wanaweza kushawishi iundwe kwa sababu zao binafsi ikiwamo kupata nafasi ya kuungana nao kuelekea Ivory Coast.

Nadhani wajumbe kutoka wizarani kama Katibu Mkuu, Saidi Yakubu, na wenzake wachache wanafaa kwenda kuiwakilisha nchi na si kujaza watu wengi ambao wanakwenda kuifanya timu kuwa na 'miruzi' mingi.

Tuache ufundi ufanye kazi yake kama ulivyofanya. Hatukatai watu kwenda Ivory Coast kushangilia timu, lakini wasiwe karibu. Tulisema tangu huko mwanzo, bila kamati inawezekana na kweli imekuwa hivyo.

# Watu wanane kati ya 100 wana homa ya ini

**Beatrice Shayo na Anjella Mndolwa (**TUDARCo**)**

WATU wanne hadi wanane kati ya 100 nchini wanakadiriwa kuwa na vimelea vya ugonjwa wa homa ya ini, jambo linalohitaji hatua madhubuti kukabili.

Aidha, serikali imeweka mkakati kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa huo kwa asilimia 90, vifo kwa asilimia 65 na maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ifikapo mwaka 2030.

Takwimu zinaonyesha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) inahudumia wagonjwa 2,000 kwa mwezi wenye matatizo mbalimbali ya mfumo wa chakula ikiwamo homa ya ini.

Akizungumza juzi Dar es Salaam katika Kongamano la Kisayansi la Afya na Magonjwa ya Ini Barani Afrika, Mkurugenzi wa Tiba Wizara ya Afya, Prof. Paschal Ruggajo, aliyemwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema ugonjwa huo unakua ndani ya nchi na barani Afrika.

Alisema ugonjwa huo ni chanzo cha ugonjwa wa saratani na ugonjwa sugu wa ini na kwamba wizara ina mpango mahususi wa kuweka pamoja magonjwa ya VVU, ngono na homa ya ini kama mpango mahususi wa kuyatokomeza.

Kutokana na ugonjwa huo kuenea kwa kasi, alisema tayari serikali imeshawapeleka wataalam kwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuongeza njia za ushirikiano na uwekezaji katika vifaa tiba.

"Ndiyo maana leo (juzi) wataalamu wengi wapo hapa. Kuna nchi 43 kutoka nchi za Afrika wamekuja kufanya mkutano nchini na hii ni mara ya kwanza mkutano huo kufanyika nchini kwetu," alisema Prof. Ruggajo.

Pia alisema hivi karibuni wamewaelimisha madaktari bingwa na wabobezi wa magonjwa ya ini na wapasuaji wa saratani ya ini, ikiwa ni sehemu ya kupambana na ugonjwa huo. "Nawaomba wananchi wajijengee tabia ya kujua hali za afya mara kwa mara kwa kupima katika vituo vya kutoa damu ambao nao wanatoa huduma ya kupima homa ya ini," alisema.

Alisema upimaji wa afya ni muhimu kwa sababu kuna uwezekano mkubwa wa ugonjwa wa homa ya ini kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambaye bado hajazaliwa na hilo nalo lipo katika mpango wao wa kutokomeza.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Afya kwa kupambana na magonjwa mengi hadi kuweka sera na miongozo ili kuepukana na maradhi hayo.

"Ugonjwa wa homa ya ini maambukizi yake yanafanana na ugonjwa wa ukimwi na ndio maana tunaendelea kuwapatia wananchi wetu chanjo, kuwepo kwa damu salama, sindano salama na wale watakaopata ugonjwa huo watapatiwa matibabu," alisema.

Prof. Ruggajo aliwataka wananchi kuacha tabia ya kufanya ngono isiyo salama, kuchangia vitu vyenye ncha kali na uzazi usio salama.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, alisema katika mkutano huo watajadili ugonjwa wa homa ya ini jinsi gani ya kuugundua na kuutibu.

Alisema MNH ni moja ya vituo vinne barani Afrika vinavyoshughulika na ugonjwa wa ini na mfumo wa chakula ambapo vituo vingine vipo nchini Morocco, Egypt, Afrika Kusini.

"Ugonjwa wa ini maambukizi yake ni makubwa zaidi ya ugonjwa wa ukimwi ni ugonjwa hatari kwa sababu mwisho wake unatokea ugonjwa wa saratani ya ini, kutokana na mkutano huu tutapata uzoefu mzuri kutoka kwa wenzetu," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Janabi, MNH ina wataalamu 13 na inaendelea kutoa mafunzo kwa wataalamu wengine.

Mwakilishi wa Misri, Prof. Manal el Sayed, alisema nchi yake inakaribia kupata cheti cha kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa wa homa ya ini.

"Tunakaribia kupata cheti cha kupunguza maambukizi kwa sababu mbalimbali ikiwemo kuwaelimisha wananchi na kutumia vyombo vya habari kwa lengo la kuelimisha kwa kutumia njia ya matangazo," alisema.

## Migogoro ya wakulima, wafugaji yamchefua DC

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

KUTOKANA na uwapo wa migogoro kati ya wakulima na wafugaji isiyo na kikomo katika kata ya Kibindu, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, ameunda kamati kutafuta ufumbuzi.

Katika Kata hiyo, wafugaji wamekuwa wakidaiwa kuhusika na matukio ya kujeruhi wakulima kwa kuwapiga mikuki na mapanga wakati na baada ya kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima.

Akiwa katika mkutano wake na wananchi, Okash alisema migogoro hiyo na tuhuma zinazotolewa dhidi ya wafugaji inatakiwa kushughulikiwa kwa haraka kabla hayajatokea madhara makuba.

"Serikali haiwezi kumbagua mtu. Haiwezekani kuvumilia vitendo vya kukata watu mapanga na wanaohusika kwenye matukio ya kujeruhi tutafanyia kazi kila tuhuma na hatua za kisheria kwa watakaobainika zitachukuliwa" alisisitiza Okash.

Mbali na kuunda kamati iliyohusisha wakulima na wafugaji alisema kuna oparesheni itafanyika kuwaondoa wafugaji ambao ni wavamizi katika kata hiyo ambao wanatuhumiwa kuhusika na migogoro inayoendelea.

" Baada ya kuunda kamati itakayohusika na kusuluhisha migogoro, kitakachofanyika sasa ni faini kwa wafugaji wanaolisha mifugo kwenye mashamba hazitakuwepo badala yake mifugo itakayokutwa shambani itagawanywa, itachukuliwa na itauzwa kufidia hasara na mingine itauzwa na fedha zitatumika kufanyia maendeleo sehemu husika," alisema Okash.

Mkuu huyo wa wilaya alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhani Possi, kupelaka Sh. milioni moja kukamilisha ujenzi wa machinjio ya Kata hiyo ili wananchi wapate kitoweo kutoka sehemu salama.

Awali, mkazi wa Kibindu, Tibis Athumani, alisema kwenye mkutano huo kwamba mifugo inachinjwa katika maeneo ambayo si salama kwa afya, hivyo kuomba serikali iingilie kati.




Mwenyekiti wa kampuni ya Seiko Epson Corporation, Minoru Usui akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lumumba Zanzibar, wakati uongozi wa kampuni hiyo, ulipotembelea miradi wanayoisaidia kupitia vituo vya mafunzo ya elimu ya teknolojia kwa walimu na wanafunzi visiwani humo mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatangaza kampeni chanjo polio

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kuanza kampeni maalum ya utoaji wa chanjo ya matone dhidi ya polio kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka minane kwenye mikoa sita iliyo hatarini kupata mlipuko wa ugonjwa huo.

Kampeni hiyo itafanyika kwa siku nne kuanzia Septemba 21 hadi 24, mwaka huu, na inalenga kuwafikia watoto 3,250,598 waliozaliwa baada ya mwaka 2016 ili kuwakinga dhidi ya kirusi cha polio aina ya pili kinachosababisha ulemavu wa kudumu.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, alisema chanjo hiyo itahusisha mikoa ambayo inapakana na nchi zenye mlipuko wa polio ambayo ni Rukwa, Kagera, Kigoma, Mbeya, Katavi na Songwe.

Alitaja idadi ya watoto wanaotarajiwa kufikiwa na chanjo hiyo kwenye mabano kuwa ni Rukwa (391,883), Kagera (729,387), Kigoma (884,477), Mbeya (614,346), Katavi (227,862) na Songwe 402,643.

Ili kufanikisha kampeni hiyo, alisema wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wadau wa chanjo imeshafanya maandalizi kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa chanjo bila kuathiri shughuli zingine za wananchi.

"Aidha, wakati wa kampeni kutakuwa na jumla ya timu yenye watoa huduma za afya 5,291 kwa mikoa yote sita itakayofikiwa na zoezi hili ambapo kila timu itakuwa na watoa huduma watatu," alisema.

Alibainisha kuwa timu hizo zitakuwa zinatoa huduma ya chanjo kwa walengwa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya, nyumba kwa nyumba, shuleni na maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ikiwamo nyumba za ibada.

Ummy aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya za Tanzania Bara zitakazohusika na chanjo hiyo kusimamia kwa karibu maandalizi na utekelezaji wa kampeni kupitia Kamati za Afya ya Msingi ngazi za mikoa na wilaya.

Aliwaelekeza waganga wakuu wa mikoa na halmashauri kuhakikisha upatikanaji wa chanjo, vifaa na mafunzo kwa wataalam watakaohusika katika utoaji wa chanjo. Pia alitoa rai kwa wazazi na walezi kutoa ushirikiano kwa watoa huduma za afya ili kuwezesha watoto wao kuchanjwa kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba.

Awali, Ummy alisema Mei 26, 2023, wizara ilipokea taarifa za uwapo wa mtoto mmoja mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi kumi na moja ambaye alionyesha dalili za kupooza kwa ghafla.

"Mtoto huyu alitolewa taarifa kutoka Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa na uchunguzi wa maabara ulithibitisha kuwa mtoto huyu ana maambukizi ya virusi vya Polio.

"Maambukizi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa polio yametolewa taarifa katika nchi zinazopakana nasi mfano Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia," alisema.

Alibainisha hali hiyo inaongeza tishio na hatari ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Polio nchini hususan kwenye mikoa hiyo.

Aidha, alisema watoto tisa kati ya kumi wenye maambukizi ya ugonjwa wa Polio huwa hawaonyeshi dalili. Vilevile, mmoja kati ya watoto mia mbili wenye maambukizi hupata ulemavu wa kudumu.

"Kutokana na tishio lililotajwa hapo juu pamoja na ukaribu wa kijiografia na mwingiliano mkubwa wa watu uliopo kati ya nchi yetu na nchi zenye mlipuko wa ugonjwa wa polio hivi sasa," alisema.

# Jafo asisitiza utekelezaji makubaliano ya Paris kuleta uhimilivu kwenye chakula

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amezisisitiza nchi za Afrika kuzibana nchi zinazoendelea kutekeleza Makubaliano ya Paris ya kuzisaidia kifedha ili zitumike kukabiliana kuleta uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika kilimo.

Amezitaka nchi hizo zinapokwenda kwenye Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) kuwa na msimamo mmoja na mfumo shirikishi wenye lengo la kuhakikisha kunapatikana fedha na teknolojia ili kuboresha mfumo wa chakula na ukuaji sekta ya kilimo.

Akizungumza jana katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), Dar es Salaam, Waziri Jafo alisema changamoto zinazoikumba sekta ya kilimo Afrika ni ukosefu wa mfumo sahihi wa kifedha wa teknolojia ya uhimilivu katika sekta hiyo.

"Sasa hivi tuna changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, kila utakapo kwenda hapa nchini utakutana na kesi za mifugo kufa na mazao kutostawi ipasavyo,kwa hiyo kama tulivyokubaliana kwenye mkataba wa Paris, suala hili lazima litiliwe mkazo, lazima watimize ahadi waliyoitoa" alisisitiza Dk. Jafo.

Alizitaka nchi hizo zisiuchukulie mkutano huo kama sehemu ya kustarehe bali sehemu ya kushinikiza Makubaliano ya Paris yatekelezwe ili zipatikane fedha za kuwekeza katika teknolojia ya kisasa kuboresha mifumo ya chakula ikiwamo kilimo, mifugo na ufugaji.

Alisisitiza kuwa Afrika si mzalishaji mkubwa wa hewa ya ukaa inayosababisha uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi lakini ni mwathirika mkubwa kutokana na kutokuwa na mifumo sahihi ya fedha na teknolojia inayohimili mabadiliko ya tabianchi.


Kwa mujibu wa Jafo, hatua ya mabadiliko hayo ndiyo chanzo cha mvua kutonyesha ipasavyo Afrika, hivyo ni lazima kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Tanzania imeanza kwa kutenga zaidi ya Sh. bilioni 214 kwa ajili ya uwekezaji katika sekta hiyo.

"Hata mradi huu wa BBT na kusaidia wakulima kuwapo mbolea ya ruzuku ni hatua nyingine, nasisitiza haja ya kuwa na kauli moja kwa nchi za Afrika ili kuhakikisha wenzetu wanasaidia sekta ya kilimo sio kama hisani bali ni wajibu wao na haki yetu hatua ambayo italeta uhimilivu sekta ya chakula,"alisema.

Aidha alisema serikali pia inachukua juhudi za kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za binadamu kama vile kilimo na ufugaji usio na tija ikiwamo kutoa elimu kwa wakulima.

Kuhusu wafugaji wanaoharibu mazingira wakati wa kuhamisha mifugo, Jafo alisema tayari utaratibu unafanyika ikiwamo hatua za haraka za kupeleka huduma za kijamii katika maeneo ya wafugaji ili kudhibiti ufugaji wa kuhama.

"Tumechimba malambo wilaya ya Simanjiro kudhibiti wafugaji kuhama na wenzetu Wizara ya Mifugo na Uvuvi wametengewa zaidi ya Sh. bilioni 9.9 kwa ajili ya utengenezaji wa malambo 16 ya wafugaji. Serikali imedhamiria kuwekeza miundombinu sahihi ya ufugaji,"alisema.




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wapili kulia) na Waziri wa Mifugo wa Uganda, Bright Rwamirama wakitiliana saini mkataba wa makubaliano, jijini Dar es Salaam juzi ya ushirikiano katika udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayovuka mipaka na yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama katika maeneo ya mipaka, unaolenga kutokomeza kabisa magonjwa hayo ili kuimarisha afya ya mifugo kwa pande zote mbili. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Bil. 650/- zinahitajika uzalishaji mbegu

**Na Renatha Msungu**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema zaidi ya Sh. bilioni 650 zinahitajika kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya chakula.

Pia amesisitiza kuwa serikali itatoa mashamba yenye miundombinu ya umwagiliaji kwa wazalishaji mbegu kutoka sekta binafsi hapa nchini ili kuchangia kufikia asilimia 75 ya mahitaji ya mbegu bora ifikapo mwaka 2025.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kupokea trekta kutoka kwa Kampuni ya John Deere. Trekta hilo litakabidhiwa kwa vijana watakaoshinda andiko la biashara wanalokwenda kufanya.

Bashe alisema serikali ina mashamba 17 ambayo yanaendelea kuboreshwa miundombinu ya umwagiliaji ili yaweze kutumiwa.

"Serikali ina mashamba 17 ambayo yameboreshwa na mengine yanaendelea kuboreshwa miundombinu yake, lakini hatutayatumia yote peke yetu, tutawapa na sekta binafsi ili nao watusaidie kuzalisha, lengo ni kufikia asilimia 75 ili kukidhi mahitaji ya mbegu," alisema Bashe.

Alisema ili kufikia malengo hayo serikali imejipanga kuwekeza katika kufanya utafiti katika mbegu ambazo zinaweza kuzalishwa kwa wingi katika maeneo ambayo serikali itakuwa imetoa.

Bashe alisema wanatumia taasisi za utafiti wa kilimo ili kuhakikisha wanafanya kilimo chenye tija ambacho kitatoa matokeo chanya kwa wakulima nchini.

Kuhusu trekta lililotolewa, Bashe alisema watalitoa kwa vikundi vya vijana ambao wataandika andiko linaloeleza nini wanakwenda kufanya, baadaye kutafanyika mashindano na kikundi kitakachoshinda ndicho kitapewa trekta hilo.

Alisema mchakato wa kupata mshindi utafanyika kwa ushirikiano wa Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Kimataifa ya Mifumo ya Chakula (AGRF) na litakuwa shindano la wazi ili kuhakikisha haki inatendeka katika kupata kikundi kitakachoshinda.

Alisema wanafanya hivyo kwa sababu siyo kila kijana anakwenda kulima, kuna wengine wanakwenda kufanya uzalishaji wa mbegu, wengine kazi za ugani.

Kuhusu uhitaji wa mbegu pamoja na fedha, Bashe alisema mwaka 2021 uwezo wa serikali kuzalisha mbegu ulikuwa ni chini ya asilimia 20, mahitaji, ya mbegu ilikuwa ni tani 120,000.

## Ulega ahimiza ufugaji samaki

**Na Renatha Msungu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdalla Ulega amewahimiza Watanzania kujihusisha na ufugaji wa samaki kwa sababu unalipa.

Alitoa ushauri huo jijini Dar es Salaam jana wakati akielezea fursa za uchumi wa buluu katika mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF).

"Fursa za mifugo na uvuvi ni kubwa mno, bado tunayo nafasi ya kufanya zaidi hususani katika uvuvi wa asili kwa kuweka msukumo wa ufugaji samaki," alisema.

Ulega alisema serikali inafanya jitihada kuhakikisha uvuvi wa asili kwa kufuga samaki kwa njia ya vizimba hususani katika Ziwa Victoria unapewa kipaumbele.

"Serikali imeonesha njia kuwa ufugaji wa samaki unalipa kwa kuwapa boti kubwa wavuvi na hatua hiyo imewahamasisha watu wengi kuhamasika kufanya shughuli hiyo,"alisema.

Naye Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, alisema ili kuhakikisha sekta ya uvuvi inafanya vizuri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha sera mpya ya uchumi wa buluu na kuweka mpango mkakati wa uvuvi, kuanzisha Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2022.

Alisema wamewawezesha vijana kushiriki katika uvuvi na kutengeneza vikundi visivyopungua 577 vinavyojihusisha na uvuvi mdogo, sambamba na kutengeneza boti 577 za kutekeleza shughuli za uvuvi.

"Katika shughuli za uchumi wa buluu wanayo mazao ya bahari ambayo ni mwani, ufugaji wa kaa, samaki na mazao bahari katika suala ya ufugaji tumewawezesha wafanyabiashara kuwekeza katika ufugaji eneo la Unguja na Pemba,"alisema.

Alisema mpango wao ni kujenga mabwawa 100 kwa ajili ya ufugaji wa mazao bahari na utekelezaji wake unaendelea na mwishoni mwa mwezi huu wanatarajia yote yatakuwa yamekamilika.

Hivyo, aliwataka wanaotaka kuwekeza katika uvuvi wawasili nchini kuwekeza kwa sababu kuna mazao ya bahari ya kutosha.

**"Serikali imeonesha njia kuwa ufugaji wa samaki unalipa kwa kuwapa boti kubwa wavuvi na hatua hiyo imewahamasisha watu wengi kuhamasika kufanya shughuli hiyo,"alisema.**



## HABARI DODOMA

# Bashungwa aanza na wadaiwa sugu kodi za nyumba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ameagiza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuwabana wadaiwa sugu wanaodaiwa kodi za pango zaidi ya Sh.bilioni 81 bila kumuonea aibu mtu hata kama ni kiongozi.

Aidha, ameitaka TBA kuja na mkakati wa kujenga nyumba za bei nafuu hasa kwa vijana wanaoajiriwa katika utumishi wa umma hususani mkoani Dodoma ili kumudu gharama za maisha. Alitoa maagizo hayo wakati akizungumza na menejimenti ya wakala huo jijini hapa, alisema fedha hizo zinapaswa kupatikana ili kusaidia utekelezaji wa miradi mingine nchini.

"TBA simamieni sheria kwa yeyote asiyelipa kodi hata kama ni kiongozi, waandikieni notisi ya kulipa madeni yao na wasipolipa waondoweni, wapo wengine nje wanasubiri wapewe nyumba ili waweze kulipa kodi kwa wakati na tutatumia makusanya hayo kujenga nyumba nyingine," alisema.

Kuhusu ujenzi wa nyumba za bei nafuu, Bashungwa alisema "Kuna vijana ambao wanaingia kwenye kada ya utumishi wa umma na bado hawajawa na uwezo wa kujijengea nyumba, kupitia TBA mnaweza kujenga nyumba za bei rahisi kwa ajili ya vijana hao ili kuwarahisishia gharama za maisha."

Hata hivyo, aliusisitiza wakala huo kuwa na utaratibu wa kuwajengea uwezo wataalamu walionao ili kuenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya teknolojia hasa katika suala la ujenzi na uendelezaji wa majengo mbalimbali.

Naye, Mtendaji Mkuu wa TBA, Daud Kondoro, alisema kuwa wakala huo utahakikisha unatafuta ufumbuzi wa vikwazo vilivyopo na kumuahidi Waziri Bashungwa kuandaa mikakati mizuri itakayosaidia wakala huo kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alieleza kuwa hadi sasa TBA inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 3,500 za watumishi wa umma eneo la Nzuguni Dodoma ambapo awamu ya kwanza ya nyumba 150 utekelezaji umefikia asilimia 95 na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 150 utekelezaji wake umefikia asilimia 10.

Alisema: "Miradi mingine ni ujenzi wa nyumba 20 za viongozi jijini Dodoma ambazo zililenga kukabiliana na uhaba wa nyumba za viongozi baada ya serikali kuhamia Dodoma ambapo mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na nyumba zimeanza kutumiwa na viongozi".



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiagana na baadhi ya wabunge, baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Maofisa Ustawi wa Jamii tekelezeni majukumu kwa ufanisi'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, amewataka maofisa ustawi wa jamii kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ili kuwa na jamii yenye ustawi mzuri.

Akifunga mkutano wa mwaka wa kiutendaji wa maofisa hayo jijini hapa, Naibu Waziri huyo alisema maofisa hao wana dhamana kubwa kuhakikisha usalama na amani ndani ya jamii.

Aliihakikishia serikali itaendelea kuboresha mazingira, miundombinu na huduma ili wafanye kazi kwa ufanisi.

"Ajenda hii ni muhimu na imebebwa kwa uzito na viongozi wetu wa kitaifa hususani Rais Samia Suluhu Hassan, ndio maana aliunda wizara hii kwa sababu anajua changamoto, malengo, matatizo ya Watanzania, hivyo maofisa mliopo hapa mtakuwa mabalozi wazuri kwa wananchi, muwapokee, mtatue matatizo yao, wajue kwamba serikali yao ipo inafanya kazi," alisema.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Seif Shekalaghe, alisema maofisa hao ni kada muhimu sana kwa jamii kwa kuwa matatizo mengi yanayotokea hasa ukatili wa kijinsia yanatokana na uwepo wa matatizo ya kisaikolojia hasa afya ya akili.

"Sisi makatibu wakuu na ninyi maofisa ustawi wa jamii ndio watekelezaji wa mambo yote kwa wananchi naamini tukionesha mshikamano nawahakikishia kuwa malengo yetu ya kuwahudumia wananchi yatakuwa yametimia,"alisema.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI (Afya), Dk. Wilson Charles, alisema ofisi hiyo itashirikiana na mamlaka nyingine kuhakikisha inatatua kero mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwamo uhaba wa maofisa wa vitendea kazi katika kuwahudumia wananchi.

# Luhemeja ahimiza watendaji kutangaza mafanikio ya wizara

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATENDAJI wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana Ajira na Wenye Ulemavu wametakiwa kutangaza mafanikio ya wizara na taasisi zake ili wananchi kutambua fursa zinazowezeshwa na serikali.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alitoa kauli hiyo jana kwenye kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya wizara na taasisi zilizopo chini ya ofisi hiyo, kilichofanyika jijini hapa.

Alisema ni muhimu kutumia vyombo vya habari kuzungumzia namna ofisi hiyo inavyo ratibu, kusimamia na kukuza sekta ya kazi, maendeleo ya vijana, ajira na ustawi wa watu wenye ulemavu.

"Ziandaliwe programu maalum kupitia vipindi vya elimu kwa umma vitakavyoelimisha wananchi kuhusu fursa pamoja na majukumu mengine muhimu yanayotekelezwa na serikali kupitia ofisi hii," alisema.

Naye, mchoraji katuni na mdau wa vijana, Ali Masoud (Kipanya) alisema yupo tayari kushirikiana na ofisi hiyo kutangaza mafanikio yanayofanywa na serikali katika kukuza ustawi na maendeleo ya vijana nchini.

# Wenye maambukizi ya VVU watakiwa kutotupa dawa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka watu wote ambao wanatumia dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya Ukimwi (ARVs) nchini kuacha tabia ya kukatiza dozi hata kama watapimwa na kukutwa hawana maambukizi.

Majaliwa alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza kwenye kilele cha mdahalo wa kitaifa ulioandaliwa na Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi Tanzania (NACOPHA).

Alisema hawapaswi kuacha matumizi hata kama watapima na kubaini kuwa hawana maambukizi ya VVU isipokuwa kwa ruhusa ya wataalam wa afya.

"Kuna watu walishawahi kupima wakakutwa hawana maambukizi wakaacha dawa ghafla hali ambayo iliwapa wakati mgumu, hivyo basi wote mnaotumia dawa hizi mnapaswa kutoacha kutumia hadi mtakapo elekezwa na wataalam wa afya," alisisitiza Majaliwa.

Alisema kitendo cha wagonjwa kuacha dawa bila kupata maelekezo kutoka kwa wataalam wa afya ni hatari kwa afya zao.

Aidha, alisema serikali inaendelea na jitihada za kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza afua mbalimbali za masuala ya UKIMWI.

"Kutokana na usimamizi mzuri wa serikali katika masuala ya VVU na UKIMWI nchini, tumeweza kuvuka malengo ya kufikia asilimia 95 ya watu wanaotumia dawa, walipima na kuanza matumizi ya dawa kabla ya kufika mwaka 2025" alisema

Kadhalika, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 inatokomeza kabisa maambukizi ya mapya ya VVU.

Naye, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alimpongeza Waziri Mkuu Majaliwa kwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wanaume kujitokeza kupima VVU.

Alisema katika jarida maarufu la kimataifa la sayansi na afya (Lancet) limethibitisha watu wanaoishi maambukizi wakitumia dawa vizuri wanapunguza maambukizi kwa wengine kwa zaidi ya asilimia 70.

Vile vile, alisema kutokana na jitihada ambazo zinafanywa na serikali kwa kuongozwa na Waziri Mkuu, idadi ya watu waliopima VVU na UKIMWI na kutambua hali zao imeongezeka kutoa asilimia 61 mwaka 2016 hadi asilimia 97 mwaka huu.

Awali, Mwenyekiti wa baraza hilo, Leticia Mourice, alipongeza serikali kwa jihada inazofanya kwa watu wanaoishi na maambukizi ya UKIMWI hali ambayo imefanya kutoka katika mazingira ya kuishi kwa matumaini hadi kuishi kwa kujiamini.



# Makamu wa Rais aagiza usimamizi maeneo ya maporomoko

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wasimamizi wa sekta ya ardhi na mazingira kuweka mipango maalum na sahihi ya kuyanusuru maeneo yote yaliyoathirika kwa maporomoko ya maji na matumizi ya binaadamu.

Alitoa maagizo hayo jana alipotembelea mashimo ya mchanga eneo la Donge Uwanda Mkoa wa Kaskazini 'A' Unguja pamoja na maporomoko ya Masingini katika Shehia ya Mtoni ChemChemu, Wilaya ya Magharib A Unguja akiwa kwenye ziara maalum za kuangalia athari kwenye maeneo hayo.

Alisema kwamba Zanzibar inaendelea kuwa na miradi mikubwa ya uwekezaji na mahitaji ya rasilimali ya mchanga inaendelea kuongezeka sambamba na kuwepo athari za kimazingira jambo linalohitaji mipango sahihi katika matumizi ya rasilimali ya ardhi iliyopo.

Makamu huyo alisema kwamba ardhi iliyopo Zanzibar ni ndogo huku kukiwa na ongezeko la mahitaji makubwa lakini ni lazima kila eneo la ardhi lililopo litumike kwa tija kubwa hasa kwa vile ardhi ni miongoni mwa rasilimali zenye thamani kubwa nchini.

Aidha, alifahamisha kwamba suala la matumizi ya rasilimali za ardhi katika miradi ya kimaendeleo litaendelea kuwepo jambo linaloweza kusababisha kuwepo tatizo kubwa la kimazingira iwapo wataalamu hawakutumia uwezo wao katika kuweka mipango bora inakayosaidia kupunguza hali hiyo.

Aliwataka wataalamu kufikiria mbinu mbadala kuyakuza maeneo yenye changamoto ya namna hiyo kuwa fursa kwa kubuni ili kuweza kuanzishwa miradi mbadala itakayochangia uchumi wa wananchi na taifa kwa jumla.

Othan pia alivitaka vyombo mbalimbali kuhakikisha kwamba wanazuia uchimbaji wa mchanga pamoja na ujenzi katika njia zisizo rasmi kwa vile inaweza kuchangia kuongezeka kwa athari zaidi zinazotokana na hali hiyo.

Pia aliziagiza mamlaka hizo kuhakikisha wanaweka alama maalum kwenye maeneo yote hatarishi ambayo yametumika kwa rasilimali hizo, ili kuzuia maafaa ya vifo kama ilivyotokea huko katika eneo la machimbo ya mchanga Donge Muada na kusababisha vifo vya watoto wanne.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Zanzibar, Joseph John Kilangi, alisema kwamba maafa yaliyotokea ya kufariki watoto watatu waliozama kwenye maji yaliyotwama katika mashimo ya mchanga huko Muanda miezi michache iliyopita lazima iwe fundisho kwa vyombo vinavyosimamia rasilimali hiyo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayubu Mohammed Mahamoud, alisema serikali ya mkoa huo itahakikisha inaweka mipango na utaratibu sahihi utakaozuia athari yakiwemo maafa kutokana na uchimbaji wa mchanga.

Mkuu wa Wilaya ya Magharib 'A', Suzan Piter Kunambi, alisema eneo la Mtoni Chemchem limeathirika sana kimazingira na tayari miti mingi mikubwa imeng'oka kutokana na shughuli za kibinaadamu ukiwemo uchimbaji wa mchanga na ujenzi katika njia zisizo rasmi.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdulla Said (kulia) na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Rok Development ya Uturuki, wakionyesha hati ya makubaliano Unguja jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa ujenzi wa shule za ghorofa Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yabariki mafunzo ya huduma za viwanja vya ndege

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema inaunga mkono mpango ulioandaliwa na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST) katika utoaji wa mafunzo ya huduma za viwanja vya ndege .

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Khamis Abdalla Said, alisema hayo alipokuwa katika hafla ya utiaji saini makubaliano ya utoaji wa mafunzo hayo kwa Taasisi ya Karume na wataalamu wa huduma za ndege katika viwanja vya ndege.

Alisema hatua hiyo inakwenda sambamba na dhamira ya Serikali juu ya kuimarisha usafiri wa anga nchini.

Aidha alisema kuwepo kwa mafunzo hayo kutachochea kupatikana wafanyakazi wa kutosha wenye utaalamu wa kutoa huduma kwa kiwango kinachohitajika.

Alisema vijana wengi wanamaliza elimu na kubakia mitaani kufanya mambo yasiostahiki, hivyo kutokea kwa mafunzo hayo ni chachu ya kutimiza ndoto zao na kuipunguzia mzigo serikali.

Hata hivyo alisema Zanzibar inaendelea kujenga miundombinu na kujenga viwanja vya ndege Unguja na Pemba, hatua ambayo itasaidia kuongeza idadi kubwa ya ndege kutoka nchi mbalimbali.

Aidha, alisema kutokana na hali hiyo KIST inajukumu la kuhakikisha wanaandaa wataalamu wataokuwa na uweledi ambao wataweza kufanya kazi hizo ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST), Dk Mahmoud Abdulwahab Alawi, alisema wamesaini makubaliano hayo kwa ajili ya kuendesha kozi tofauti za utoaji wa huduma kwa kazi zinazofanyika katika viwanja vya ndege.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwajengea uwezo wazawa kufanya kazi hizo kutokana na kuwepo idadi kubwa ya viwanja vya ndege na kampuni mbalimbali kufanya safari zake nchini.

Mkuu wa Idara ya Uhandisi wa Mitambo na Usafiri wa Anga kutoka Taasisi ya Karume, Ali Hamad Mkali, alisema lengo la makubaliano hayo ni kuanzisha mafunzo ya muda mfupi ndani ya taasisi hiyo kwa lengo la kuwaandaa vijana ili kuingia katika soko la ajira kupitia eneo hilo la utoaji wa huduma katika viwanja vya ndege.

Mtaalamu wa mafunzo hayo, Hassan Ngozi, alisema watoa huduma za ndege wanahitajika kuwa na taaluma na uelewa ili kuepusha athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza.

## Polisi wapewa mbinu ufuatiliaji matukio, kuondoa malalamiko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani, Kaspar Mmuya, amewataka askari wa Jeshi la Polisi kwenda na wakati na mfumo wa kielektroniki ambao kwa kiasi kikubwa utaondosha malalamiko na kufuata matukio yanayojitokeza kwa ufanisi mkubwa.

Aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya uongozi mdogo wa sajenti kwa askari wa jeshi hilo 774 makao makuu wa jeshi hilo mjini Unguja.

Alisema mfumo wa kisasa wa kielektroniki utakaotumiwa na Jeshi la Polisi utaongeza ufanisi na kupambana na matukio ya rushwa ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wananchi dhidi ya jeshi hilo.

Hivyo, aliwataka wapiganaji hao waliomaliza mafunzo ya ngazi za awali ya sajenti kuonesha uwezo wao na kuyatumia mafunzo waliyoyapata na kuwa chachu ya kuleta uwajibikaji na ufanisi.

Aidha, aliwataka wahitimu hao kufahamu kwamba rushwa ni aduai wa haki na miongoni mwa mambo ambayo yamekuwa yakitiliwa mkazo katika kuyatokomeza katika Jeshi la Polisi ambalo miongoni mwa majukumu yake ni kufuatilia haki.

Naye Kamishna wa Jeshi la Polisi (Utawala na Rasilimali Watu), Suzan Kaganda alisema Jeshi la Polisi litaendelea kusimamia haki na utawala bora katika utendaji wake.

Aidha, aliwataka wahitimu hao kujiendeleza kwa kutumia fursa na nafasi mbalimbali zinazopatikana kwa ajili ya kujiweka tayari kwenda na ufanisi wa utoaji wa huduma.

Kamishna Mkuu wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad aliwataka askari wa jeshi hilo kuhakikisha kwamba wanapambana na uhalifu katika maeneo yote ikiwemo katika ulinzi wa sekta ya utalii Zanzibar.



**50 CENT ONA ULIVYOKOSA BUSARA** Ukurasa 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT

JUMAMOSI SEPTEMBA 9, 2023



# MWANAKULITAFUTA....

KUNA ule msemo unaosema mwanakulitafuta mwanakulipata! Ndivyo kwa sasa unashabihiana na mazingira anayokabiliana nayo rapa mwenye utata, Nay wa Mitego.

Wiki hii msanii huyo amejikuta akipamba vichwa vya habari baada ya kujisalimisha polisi kutokana kile kinachoelezwa maudhui ya kibao chake 'Amkeni' kuwa na chembe za uchochezi.

Nay wa Mitego, alifika kituo cha Polisi Kati, baada ya kutakiwa kufanya hivyo na jeshi hilo.

Wimbo huo umekuwa na utata tangu ulipotambulishwa baada ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutangaza kuufungia na Baraza la Sanaa Tanzania kumuamuru msanii huyo kufika ofisini ili kujieleza.

Hata hivyo inaelezwa msanii huyo alifanya ukaidi baada ya kutotokea kwenye ofisi hizo, badala yake aliendelea kufanya shughuli zake za kimuziki mikoani.

Ukaidi huo alioufanya dhidi ya mamlaka unadaiwa kuonekana kama mwendelezo wa kiburi na ukaidi wa msanii huyo.

Sio mara ya kwanza kwa msanii huyo kuingia katika mvutano na serikali kutokana na tungo zake, miaka minne iliyopita alikamatwa na polisi mkoani Morogoro mara baada ya kutoa ngoma yake 'Wapo'.

Hata hivyo, Nay wa Mitego hakutaka kufafanua zaidi kuhusu nini anacholalamikiwa hadi kutakiwa kuripoti polisi, lakini alikiri wimbo wake 'Amkeni' ndio umemletea tatizo hilo.

"Sitaki niongee zaidi lakini mimi ni sauti ya watu, kukamatwa kwangu ni sawa nilivyo kamatwa miaka minne iliyopita baada ya wimbo wangu wa 'Wapo' kutoka," alisema.

BASI SAWA

## 'Huku' imeleta mapinduzi

VIDEO ya wimbo mpya wa Ali Kiba na Tommy Flavour unaoitwa 'Huku' imeibua mjadala baada ya wasanii hao kutoonekana na badala yake watangazaji wa vituo vya redio pekee wametumia kuinogesha.
Katika video hiyo Ali Kiba na Tommy Flavour wamesikika sauti pekee, huku wanahabari wa vituo vya Clouds fm, East Africa Radio na EFM wakiipamba vilivyo.
Idadi kubwa walioitazama wametoa pongezi kwa wasanii hao kutokana na ubunifu wao kiasi ambacho mtu anapoitazama hawezi kukinai kwa haraka.



## Asihukumiwe Mavoko

KUNA maoni tofauti tofauti baada ya video ya msanii wa Bongo Fleva, Rich Mavoko, kusambaa akionekana akiwaburudisha watu mtaani.
Video hiyo ambayo ilianza kusambaa Jumatano ameonekana mwanamuziki huyo akiimba kwenye uwanja wa vumbi huku watu wachache wakimsikiliza na kumtunza pesa.
Baadhi wa watu walitoa maoni kuhusu video hiyo, walisema hatua aliyofikia msanii huyo kwa sasa anatakiwa kupewa msaada wa ushauri kutokana na kuharibu hadhi yake.
Wengine walimuunga mkono kwa kueleza anachokifanya ni jambo la kawaida kwa sababu burudani hutolewa mahali popote ili mradi apate mapato yake.





## Paula ametania au...

KAMA ulikuwa utani kutoka kwa Paula, basi umezusha balaa na kumchongea mpenzi wake ambaye ni msanii wa kizazi kipya Marioo.
Marioo ambaye kwa sasa anafanya vizuri kwenye muziki wa Amapiano, eti anadaiwa kutoa mahari ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya kumuoa binti huyo ambaye mama yake ni mwigizaji Kajala Masanja.
Paula alifichua hayo katika video moja iliyosambaa mitandaoni, akisema japo kwa utani kwamba Marioo kashalipa mahari yenye kitita hicho cha pesa.
Hata hivyo, bado haijatibitishwa kauli hiyo ya Paula ambayo imesababisha watu kupigwa na butwaa kutokana na kiasi kikubwa cha pesa ya mahari kama ni kweli ameitoa.



## Bibi Fatuma: Usiamini vicheko

**Na Adam Fungamwango**

UCHUNGUZI ni muhimu kwa kila unachoambiwa. Siyo kila unachoambiwa basi ni kweli, hata kutoka kwa watu ambao unawaamini. Inawezekana na wao wamelishwa au kuaminishwa linalozungumzwa. Kila unachoambiwa kama huna uhakika nacho inabidi ujipe muda wa kukitafakari na kujipa muda wa kuchunguza na hatimaye kupata ukweli ili kujipa majibu ya kweli.
Filamu hii iitwayo 'Bibi Fatuma' inakufundisha kitu kuanzia leo kuwa 'usiamini vicheko.'
Waliocheza filamu hii ni Sikudhani Mohamed, Isihaka Ramadhani, Bi. Kwega, Sabitina Omar, Athuman Bama na wengine.
Yaani siyo kila kinachozungumzwa ni kweli, huenda nyuma yake kuna tatizo.
Nasri anataka kuoa. Amepata mchumba mtaani hapo anaitwa Fatuma, au Fetty.
Barua inapelekwa. Sare zinasambazwa na watu wanaalikwa. Fatuma mwenyewe anajishebedua kwa watu kuwa anakwenda kuolewa huku shoga zake wakiwa wanaendelea kubaki majumbani kwao.
Benga ambaye ndiye mshenga kwa muda mrefu ameshindwa kupeleka mrejesho na nini kinakwamisha.
Fatuma mwenyewe na bibi yake wameingia na hofu kwani hawajui tatizo ni nini.
Nasri naye anashindwa kujua kwa nini mshenga wake ambaye amekuwa kiunganishi amekuwa ni kama hafuatilii suala hilo. Kumbe amekuwa akila rushwa kwa mtu fulani asiifanye hiyo kazi.
Kaka yake Nasri aitwaye Mpayu anamwambia mkewe kuwa hataki kabisa mdogo wake huyo amuoe Fatuma kwa sababu bibi yake ni mchawi.
Hilo ndilo linaloanza kuenea mtaani hapo kuwa bibi Fatuma ni mchawi ndiyo maana kaka yake Nasri, Mpayu amemkataza kumuoa.
Kumbe watoto wa Mpayu kuna siri wamekaa nayo moyoni kwa muda mrefu wakihofia ugomvi baina ya wazazi wao.
Walitoka shuleni na kumkuta Fatuma chumbani akiwa na baba yao Mpayu. Dogo wa kiume yeye akaamua kumwambia baba yake mdogo Nasri.
Nasri akamwambia rafiki yake Bama ambaye alikwenda kulibwaga kwa mke wa Mpayu.
Siri ikafichuka kuwa kumbe Mpayu anatembea na mchumba wa mdogo wake Nasri, Fatuma na ndiyo maana anapinga mdogo wake asioe kwa kumhonga mshenga asipeleke taarifa kwa pande zote mbili.
Mke wa Mpayu baada ya kujua hilo anaamua kubeba virago vyake na kuondoka, Fatuma yeye kwa sababu tayari alishajua anakaribia kuolewa, lakini ikagundulika kuwa ana uhusiano wa kimapenzi wa shemeji yake, akaamua kujinyonga.





## Chege amshauri Nature

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, Chege amesema kuna watu wanamyumbisha Juma Nature kiasi ambacho anatoa maneno yenye mihemuko.
Chege amesema hayo baada ya Juma nature kueleza kwamba hakutokea katika tamasha la muziki la wasafi lilofanyika Mtwara kutokana na yeye sio msanii wa kulipwa shilingi laki tano.
Amesema kilichozungumza hakitokani na Juma Nature, bali ni watu waliokuwa nyuma yake ambao wanamyumbisha na kumpa mwelekeo mbaya.
"Tuna kazi nyingi tumefanya na wasanii wa wasafi ambazo zinakuja, huku ni kumrudisha nyuma na ni lazima kutafakari kabla hujasema jambo," amesema.

## Mwezi Septemba umedamshi ngoma

**Na Adam Fungamwango**

MWEZI Septemba umeingia kama kawaida kabla haujafika katikati, tayari wasanii wameshauchangamkia kwa kutoa ngoma zao mpya.
Wasanii hao wakiwemo, Ali Kiba, Zuchu na wengineo wametambulisha ngoma zao mpya mwanzoni tu mwa mwezi huo ambazo taratibu zimeshaanza kuteka mioyo ya mashabiki wa muziki wa bongo fleva, nazo ni hizi hapa.

**Why-Zuchu ft Haitham Kim**
Picha linaanza tu, Septemba Mosi, Zuchu amefyatua ngoma yake aliyoiita 'Why' ambayo ameshirikiana kuimba na hayati Haitham Kim.
Haitham aliyefariki Septemba Mosi, na siku hiyo hiyo ndiyo ngoma ya 'Why' ilitambulishwa.
Ina maana aliirekodi kabla ya kifo chake, mpaka anafariki mwenyewe alikuwa hajaisikia redioni wala kuiona kwenye televisheni.
Hali hii huwakuta wasanii na wanamuziki wengi duniani ambao wanarekodi nyimbo au filamu, lakini wakati zipo kwenye 'mixing', wanaaga dunia.

**Bobea- Joh Makini**
Mwimbaji wa nyimbo za kufokafoka, Joh Makini Septemba 2 alitoka na ngoma aliyoiita 'Bobea', akionekana hakutaka mwezi huu umpite hivi hivi.

**Mjinga 'remix'-Zee Cute, ft Kontawa ft Anjella**
Msanii wa kike Zee Cute, yeye akaipua ngoma yake aliyoiita "Mjinga Remix', akimshirikisha mwenzake Anjella na msanii na kiume, Kontawa.
Ngoma hiyo akaitoa Septemba 6 na imeshaanza kupagawisha kwenye makasino na kumbi mbalimbali za starehe.

**Sitoboi-Godcho Boy**
Siku hiyo hiyo, msanii mwingine, Godcho Boy yeye akafyatua ngoma yake aliyoiita 'Sitoboi' na imeanza kufanya vizuri kwenye mtandao wa instagram.

**Huku-Ally Kiba ft Tommy Flavour**
Ali Kiba alifunga kazi siku hiyo ya Septemba 6 na yeye alipopandisha ngoma yake aliyoiita 'Huku.'
Alichoua kabisa kwenye ngoma hiyo ni video ya wimbo wenyewe ambayo imekaa 'kikomediani' zaidi, utakapoiangalia utakubaliana na mimi kuwa amekuja kivingine kwenye mauala ya 'kushuti' ngoma.



Haitham Kim



# 2Baba ukasisi unatoka moyoni

MWANAMUZIKI mkongwe wa Nigeria, Innocent Ujah Idibia, maarufu kama 2Baba, anasubiriwa na wengi kupata huduma yake ya kichungaji, pale atakapoamua kuanzisha kanisa.

Hivi karibuni 2Baba alieleza nia yake ya kuwa kasisi na kuacha muziki anaoufanya na wakati mwingine anatamani kuanzisha kanisa lake.

Ukionyesha kuwa nia yake ya kuanzisha kanisa si utani, amelitaja jina kuwa litaitwa Straight To Heaven International Church of God Nigeria Limited (STHICOGNL).

Katika ukurasa wake wa Instagram, watu waliingia kwa wingi na kumpongeza kwa nia yake hiyo na kumtaka kuharakisha kwa kuwa wanasubiri kupata huduma ya kiroho.



## Gomez ajibebisha kwa Rema?

KAULI ya mwanamuziki maarufu wa Marekani, Selena Gomez kwamba anampenda mkali wa afrobeats wa Nigeria, Rema imesababisha mjadala na wengine kufika mbali kwamba wawili hao ni wapenzi.

Gomez na Rema wamefanya kolabo ya remix ya wimbo wa 'Calm Down'.

Awali Gomez alisema alikubali kufanya kazi na Rema kwa sababu anapenda tabia yake, kisha akasisitiza anataka kumtunza.

Baada ya kauli hiyo baadhi ya wafuasi wake katika ukurasa wa Instagram, walisema ikiwa mrembo huyo kakiri kumpenda Rema, basi tayari wameanzisha uhusiano wa kimapenzi.

## Joe kumtaliki mkewe mla bata

MWANAMUZIKI wa Marekani Joe Jonas na mkewe Sophie Turner, wamefikia hatma ya kuvunja ndoa yao baada ya wawili hao kutofautiana kitabia.

Tayari Jonas amewasilisha jalada la kuomba talaka mahakamani saa chache baada ya kufichuliwa kwamba mwimbaji huyo alikuwa ameajiri wakili kushughulikia talaka.

TMZ inaripoti kuwa tofauti za maisha ya wanandoa hao zilisababisha mpasuko usioweza kurekebishwa katika ndoa yao.

Joe ana tabia ya kukaa nyumbani muda mwingi na Sophie yeye anapendelea kula bata kila siku.





## Drake ampa shabiki mil. 125

RAPA maarufu kutoka Marekani, Drake amemzawadia shabiki wake kitita cha dola 50,000, sawa na shilingi milioni 125.3 baada ya kuuza vitu vyake vya ndani ili kununua tiketi ya kuingia katika tamasha lake.

Rapa huyo mwenye asili ya Canada, aliahidi kumpatia shabiki huyo kiasi hicho baada ya kuona bango lake wakati wa onyesho lake lilofanyika Las Vegas.

Alisimamisha onyesho lake ili kusoma bango hilo lilosema "Drake, nilitumia pesa zangu za samani za ndani kwenye maonyesho yako mawili."

Drake alimwambia shabiki huyo kuwa atamlipa kwa sababu anampenda.

## 50 cent ona ulivyokosa busara

MSANII mkongwe wa Hip hop kutoka Marekani, 50 Cent anashukiwa kufanya kosa la jinai baada ya kumrushia shabiki kipaza sauti na kumpasua paji lake la uso.

Kwa mujibu wa Ripoti za TMZ, msanii huyo alikuwa akitumbuiza kwenye ukumbi wa Crypto.com huko LA ndipo alipomrushia kipaza sauti mtu huyo aliyekuwa amekaa nyuma ya jukwaa.

Rapa huyo anasemekana alirusha kipaza sauti wakati wa onyesho lake kutokana na kuchanganyikiwa kwa sababu zote zilikuwa na hitilafu.





# Utoro shuleni kwa wanafunzi jamii ya ufugaji wapungua

**Na Godfrey Mushi,** MONDULI

SHIRIKA la World Vision Tanzania (WVT), limepata matokeo chanya katika Mradi wa Maendeleo wa Kisongo/Makuyuni AP, ulioko Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, baada ya kupunguza utoro kutoka asilimia 8.4 hadi kufikia 0.5 kwa wanafunzi wa jamii ya kifugaji ya kimasai.

Jana, Mkurugenzi wa Miradi wa WVT, Neserian Mollel, akizungumza wakati wa hafla ya kuhitimisha ufadhili wa mradi huo, alisema matokeo hayo yamepatikana kutokana na mradi wa afua za lishe waliouendesha katika vijiji 13 vilivyoko Tarafa ya Makuyuni na Kisongo.

"Wazo la mradi huu wa afua za lishe shuleni, ulikuja baada ya hali halisi kuonekana mwaka jana na miaka miwili iliyopita, wakati wa tathimini ya mabadiliko ya tabianchi.

Ilionekana kulikuwa na upungufu mkubwa sana wa mvua Kisongo/Makuyuni, na hivyo kuathiri uzalishaji wa chakula. Tumeshirikiana na serikali kuwezesha na kuongeza upatikanaji wa chakula katika ngazi ya jamii, na tumejikita zaidi shuleni, maana tunajua huko ndiko ambako watoto wengi wanaathirika na walishindwa kwenda shuleni.

...Faida ya mradi huu ambao tumeuona, ushiriki wa watoto darasani umeongezeka na afya zao zimeboreka."

Mwenyekiti wa wanajamii wanaoendelea kunufaika na mradi huo, Daud Laizer, alisema mradi huo umezinufaisha kata tano za Wilaya ya Monduli, zenye vijiji 13. Kwa mujibu wa Laizer, zaidi ya watu 24,311 wakiwamo wanaume 5,592, wanawake 7,014 na watoto 11,705 walioko kata za Mswakini, Makuyuni, Esilalei, Lepurko na Sepeko ndio walionufaika na mradi huo uliotekelezwa kwa miaka 21 na World Vision Tanzania.

Aidha, Mkurugenzi wa Fedha na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa WVT, John Rich, akizungumza kabla ya kukabidhi mradi huo kwa serikali, alisema mradi huo ulioanza mwaka 2002 umetimiza miaka 21 sasa.

"Hapa tulipofia hatuwezi kusema tumefika asilimia 100, lakini tunachoweza kusema tunawashukuru wafadhili waliotembea nasi World Vision, Serikali ya Marekani, ambao wamekuwa wakifadhili mradi wa Kisongo/Makuyuni,"alisema Rich.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Joshua Nassari, akizungumza kabla ya kupokea mradi huo, alisema pamoja na kazi nzuri ambayo World Vision wameifanya kwa muda wote, bado jamii ya Kisongo/Makuyuni ina uhitaji mkubwa na matatizo mengi yanayohitaji msaada wa wadau wa maendeleo wa WVT.

"Changamoto kila siku ziko mpya, bahati mbaya sana eneo letu la Kisongo/Makuyuni ni la ikolojia ya wanyama, kuna Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Hifadhi ya Taifa ya Manyara na eneo la Mamlaka ya Ngorongoro, wanyama wanapita hapa, licha ya mabadiliko ya tabianchi kututesa.

...Wanyamapori wanatoka porini kuja kwenye makazi ya wananchi kutafuta malisho na virutibisho vingine ambavyo vimeisha hifadhini. Sasa hata hawa watu wakilima, wakati mwingine ni changamoto. Kwa hiyo kwa sababu ya haya mabadiliko ya tabianchi muendelee kuandika maandiko mengine ili mtusaidie jamani " alisema.



Mbunge mstaafu wa Jimbo la Muheza mkoani Tanga, Balozi Adadi Rajabu (kushoto aliyekaa), akimjulia hali Mwenyekiti mstaafu wa CCM wa wilaya ya Muheza, Peter Jambele (wa pili kulia) anayeumwa, nyumbani wilayani humo juzi. Kushoto ni Diwani wa kata ya Masuguru, Mohamed Baghoza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mil.20/- kujenga kivuko Kitongoji cha Elerai

**Na Anjela Mhando,** SIHA

HOFU ya wakazi wa Kijiji cha Munge kilichoko Kata ya Donyomuwa, Wilaya ya Siha, kupoteza watoto wao kwa sababu ya kukosa kivuko kwenda ng'ambo ya pili ya Kitongoji cha Elerai, sasa imetoweka, baada ya serikali kutoa Sh. milioni 20 za kujenga kivuko hicho.

Wakati wa msimu wa mvua za vuli na masika, licha ya kupitia adha hiyo kwa miaka 30, wakazi wa Munge na hasa upande wa Elerai, hushindwa kusafirisha mazao yao kutokana na magari na pikipiki, kukwama kupita kwenye eneo hilo lililopitiwa na Mto Donyo.

Wakizungumza jana, mbele ya Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya hiyo, Ally Kidunda, aliyekwenda kukagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kivuko hicho, Mkazi wa Elerai, Wilson Laizer, alisema kivuko kitasaidia wananchi kuwa na mawasiliano ya barabara kwa muda wote, kuokoa maisha ya watu na kurahisisha shughuli za kiuchumi.

Aidha, Nasupati Mollel, alisema wananchi wengi walikuwa wakilazimika kupita barabara ya kuzunguka vijiji jirani, ambako kuna umbali mrefu na kutumia gharama kubwa za nauli.

"Tulijawa hofu ya kupoteza maisha kwa kusombwa na maji, maana tumehangaika miaka mingi kuomba tujengewe kivuko katika Mto Donyo na mpaka sasa, ndio serikali imesikia kilio chetu tangu mwaka 1993. Tunaishukuru sana serikali kwa kuleta fedha hizi.

"Tunaishukuru serikali kwa sababu watoto pamoja na wananchi wa Kijiji cha Munge wamepata kivuko. Wananchi wamejitoa na kukusanya mawe lori 20 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kivuko.

...Asilimia 75 ya kivuko hiki kinajengwa kwa kutumia mawe na asilimia 25 kwa kutumia malighafi ya kiwandani."

Awali, akisoma taarifa za miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na serikali katika kijiji hicho, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Munge (VEO), Winnie Muro, alisema mradi huo wa kivuko unatekelezwa kwa mfumo wa manunuzi ya serikali.

"Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kuchimba eneo la kivuko, kuandaa mkataba wa fundi na uundaji wa kamati ya usimamizi wa ujenzi. Na mpaka sasa tumeingiziwa shilingi milioni 10. Kwa hiyo utekelezaji unaanza muda wowote kuanzia sasa," alieleza ofisa huyo.

Baada ya kukagua mradi huo, Katibu wa CCM wilayani humo, Ally Kidunda, alisema serikali itaendelea kutekeleza ilani ya CCM na kuhakikisha matatizo yanayowakabili wananchi wa wilaya hiyo yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu kama ilivyo kwa Munge.

## Sababu ufaulu somo la Hisabati kuwa chini yatajwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHAMA cha Hisabati Tanzania, kimetaja sababu inayochangia ufaulu wa somo la Hisabati kuwa chini, kikisema kunatokana na uchache wa walimu wa somo hilo pamoja na kupangiwa vipindi vingi vya kufundisha.

Vikwazo hivyo vya elimu vimo katika hotuba ya Mwenyekiti wa chama hicho, Betinasia Manyama aliyoitoa juzi, wakati wa mafunzo endelevu ya walimu kazini yanayoendelea katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

Licha ya kuwapo vikwazo hivyo, aliwataka walimu wa Hisabati kupunguza ukali na wasiingie na fimbo darasani na watumie mbinu mbadala za kufundishia kwa kuwa inasababisha wanafunzi kuchukia somo hilo.

"Kama Serikali inahitaji kulikomboa somo la Hisabati na taifa kwa ujumla nidhahiri kwamba walimu wa Hisabati hapa Tanzania hawatoshi kabisa huku idadi ya vipindi vikiwa ni vingi," alisema.

Alisema washiriki zaidi ya 233 walipatiwa mafunzo na lengo kuu la chama hicho ni kuongeza uwezo kwa walimu, wanafunzi na wadau wa Hisabati katika suala la ufundishaji na ujifunzaji kwa somo hilo.

Alisema mafunzo hayo yamelenga kuboresha mbinu mbalimbali za ufundishaji kwa walimu, kuongeza hamasa na motisha kwa walimu wa Hisabati hasa katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa miundombinu na walimu hao na kujifunza mada zenye changamoto wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

"Mafunzo haya pia yamelenga kuelimisha namna tabia ya mwalimu inayoweza kuathiri uelewa wa mwanafunzi akiwa darasani na utafiti tuliofanya tumebaini kuwa tabia ya mwalimu inaathiri sana mwanafunzi kulipenda somo la hisabati na kujifunza huku wengine wakiliacha kabisa," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, Ofisa Elimu Mkoa wa Arusha, Abel Mtupwa, alisema kwa kuzingatia sera ya serikali somo la Hisabati ndiyo nguzo kuu ya maendeleo ya viwanda.

Aidha, alisema ujenzi wa taifa na kuwa na uchumi imara na endelevu hauwezi kufikiwa, endapo ufaulu wa somo Hisabati utakuwa chini au bila ya kuweka mpango mkakati wa kuliinua.

Naye, Makamu Mkuu wa Chuo cha IAA, Dk.Cairo Mwaitete, alisema kuwa ukuaji wa uchumi duniani unawategemea sana wataalamu wa hesabu.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Staili ya wauza kahawa zamani kuzurura mtaa kwa mtaa

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA si rahisi kuona vijiwe vya kahawa miaka ya 1970, 1980 na hata 1990 kama ilivyo hivi sasa.

Siku hizi kuna sehemu maalum ya kunywea kahawa ambapo watu wengi hasa wenye umri mkubwa hukutana eneo maalum la kupiga stori za hapa na pale, zikiwemo za siasa, soka na kijamii huku wakipata kahawa.

Eneo hilo kunakuwa na mtu ambaye amepanga vitu au mabenchi na kufanya biashara hiyo.

Zamani ilikuwa si rahisi sana kuona vijiwe kama hivyo kutokana na sera za wakati huo ambapo haikutakiwa mtu au watu kukaa vijiweni au watu kukaa sehemu moja kwa muda mrefu wakipiga soga tu bila kazi.

Mkikutwa mnaweza kukamatwa na kupelekwa vijiji na maporini kama Gezaulole, Tegeta, Goba na sehemu zingine ili mkalime.

Kutokana na hali hiyo wauza kahawa walikuwa wanatembeza, yoyote anayetaka kunywa basi atamwita na kununua, anywee ndani au anywe hapo hapo.

Muuza kahawa anaweza kukuta watu mpirani au kwenye mkusanyiko wa kijamii hapo anaweza kupata muda mrefu wa kukaa, lakini siyo vijiweni kama sasa.

Hata sasa wapo wauza kahawa wanaotembeza ingawa si wengi, lakini hawafanani kabisa na wale wa zamani.

Hawa wa sasa kwanza wanavaa pensi. Ni mara chache sana kuona muuza kahawa anayetembeza wa kizazi cha sasa anavaa japo suruali.

Pensi, kandambili, au makubazi na mara nyingi wanakuwa ni vijana sana. Huwezi kumkuta muuza kahawa mwenye umri mkubwa kwa sasa.

Sasa ngoja twende kwa wauza kahawa wa zamani. Kwanza kabisa wengi wao walikuwa ni watu wenye umri mkubwa.

Zamani huwezi kuona muuzaji ana umri mdogo. Inawezekana ikawa sababu kubwa ni ukosefu wa ajira. Kijana wa zamani alikuwa na uhakika wa kupata ajira hata kama amemaliza darasa la saba, lakini pia serikali haikutaka kabisa kijana mwenye nguvu zake aonekane anafanya kazi za kuuza kahawa, karanga, korosho ni lazima tu atafutiwe kazi ya kufanya, na ikishindikana kabisa atakwenda kupewa pori ili alime.

Watu wazima waliokuwa wakifanya kazi hiyo mara nyingi wengi wao walikuwa wamestaafu kazi, au wanafanya baada ya kutoka kazini. Kwa sababu mara nyingi walianza kutembeza kuanzia saa 10:00 jioni na kuendelea, na siyo asubuhi na mchana kama hawa wa sasa.

Halafu wauza kahawa wa zamani vaa yao ilikuwa ni kama sare. Walifanana.

Walipenda kuvaa misuli, juu ni lazima avae kofia aina ya kibaraghashia, lakini wengi zaidi walipenda kuvaa kofia aina ya tunga au tarabushi. Hii ni kofia ambayo mara zote ina rangi nyekundu na ina nyuzi nyingi juu ambazo zinalalia upande mmoja.

Kwa ufafanuzi zaidi kofia hizo ni zile alizokuwa akipenda kuvaa muigizaji maarufu mzee Small wakati huo, au Mbunge wa zamani wa Musoma Vijijini, Nimrid Mkono.

Wakati vijana wa sasa wauza kahawa wanakuwa wamebeba birika ambayo limavalishwa jiko lililo chini, wa zamani walikuwa na mabirika yenye rangi kama ya dhahabu, au shaba, na hayakuitwa birika bali ni deli.

Madeli wa kahawa yalikuwa manene chini, lakini kwa kwenda juu yalikuwa yakipungua unene na juu yalikuwa yamechongoka kama inavyoonekana kwenye picha.

Vikombe ni vile vile hadi leo, lakini wauzaji wa zamani walivaa fulana na sendo, msuli na walikuwa wakifanya kazi ya kupita mitaani kuuzia watu.

Ili ujue kama anapita, wengi wao walikuwa wakipigapiga vikombe vile vidogo vya kunywea kahawa ambavyo vilikuwa vikitoa mlio mkali uliokuwa unaashiria kuwa muuza kahawa anapita.

Ugongaji wake ulikuwa ni wa hali ya juu kiasi cha kuwa kivutio si kwa wanaokunywa kahawa lakini hata watoto ambao walikuwa hawanywi.

Watoto walikuwa wanamfuata muuza kahawa kwa sababu tu ya kuvigonga vikombe viwili alivyokuwa amevishika mkono wa kushoto, huku wa kulia akiwa amebeba deli.

Wauzaji wa sasa hao mpaka uwaite, bila ya kuwa na ubunifu wa ziada.

Hiyo ndiyo staili ya wauza kahawa wa zamani ambao walionekana kama ndugu kutokana na kufanana aina yao ya uvaaji wakati wakifanya kazi hiyo.

**Tuma meseji 0716 350534**




Hii ni sehemu ambayo watu wanakusanyika kunywa kahawa maarufu kama 'kijiwe cha kahawa.'



Hili ni deli la kahawa lililokuwa linatumiwa na wauzaji wa zamani ambalo lipo tofauti na mabirika yanayotumiwa na wauzaji wa sasa.



Kofia aina ya tarabushi ambayo pamoja na kuvaliwa na watu wengi huko nyuma, lakini ilipendwa zaidi kuvaliwa na wauza kahawa wa zamani.

## Mpinzani ateuliwa waziri mkuu Gabon

**RIBREVILLE,** GABON

UTAWALA wa kijeshi nchini Gabon umemteua kiongozi wa zamani wa upinzani, Raymond Ndong Sima, kuwa waziri mkuu wa serikali ya mpito.

Uteuzi huo ulifanyika Alhamisi na ulitangazwa kwenye televisheni ya taifa.

Sima, mwanauchumi mwenye miaka (68), alikuwa mkosoaji mkubwa wa Rais Ali Bongo aliyeondolewa madarakani.

Aliwahi kuwa waziri mkuu katika serikali ya Ali Bongo kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2014.

Alijiuzulu 2014 na kugombea urais 2016 na kwa mara nyingine tena mwaka huu chama chake kilikuwa sehemu ya muungano wa upinzani.

Kiongozi wa kijeshi wa Gabon Jenerali Brice Oligui Nguema, aliahidi kuleta mageuzi ya kiuchumi na ataandaa uchaguzi huru na wa haki, lakini hakusema lini utafanyika. **DW**

## Marekani yawapanga upya wanajeshi Nchini Niger

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeanza kuweka mkakati wa kuwapanga upya wanajeshi wake walioko nchini Niger kama njia ya tahadhari.

Wizara ya Ulinzi wa Marekani imetangaza juzi kuwa idara ya Ulinzi inapanga upya sehemu ya wafanyakazi wake na vifaa vyake kutoka kituo cha anga cha 101 ambacho kiko mji mkuu wa Niamey.

Kambi ya 101 inapatikana eneo la Agadez, Kaskazini mwa mji huo.

Msemaji wa Pentagon, Sabrina Singh, aliwaambia waandishi wa habari kuwa kwa sasa hakuna tishio kwa wanajeshi wake.

"Hakuna tishio limeshatokea kwa wafanyakazi wetu au chokochoko yoyote dhidi yao," alisema.

Singh pia alisema kwamba baadhi ya wafanyakazi wasio wa lazima na wakandarasi waliondoka nchini humo wiki kadhaa zilizopita.

Wanajeshi walimpindua Rais wa Niger Mohamed Bazoum, mnamo Julai 26 na kumweka kizuizini yeye na familia yake.

Marekani ina wanajeshi 1,100 nchini Niger, ambao wamekuwa wakiendesha operesheni zao dhidi ya makundi ya kijihadi yanayoendesha harakati zao katika eneo hilo. **RFI**

# Korea Kaskazini yaishtua dunia, yaunda manowari ya nyuklia

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

KOREA KASKAZINI imeishtua dunia baada ya kuzindua manowari yenye uwezo wa kubeba silaha za nyuklia.

Rais wa nchi hiyo,Kim Jong Un, alihudhuria hafla ya kuzindua manowari hiyo mpya, ambayo inadaiwa ina nguvu ya kubeba silaha za nyuklia na kulenga sehemu husika.

Ripoti katika vyombo vya habari vya serikali ilisema manowari hiyo iliimarisha kizuizi cha nyuklia cha nchi hiyo kwa kuvuka mipaka.

Nyambizi inayofanya mashambulizi ya nyuklia kwa muda mrefu imekuwa kwenye orodha ya silaha ambazo Korea Kaskazini ilitaka kuunda.

Katika picha zilizotolewa na vyombo vya habari vya serikali, ilimuonyesha Rais Kim amesimama karibu na meli akiwa amezungukwa na maafisa wa jeshi la majini, na kuambatanishwa na nyambizi kubwa nyeusi, ambayo ripoti ilidai kuwa inaweza kurusha silaha za nyuklia.

**BBC**



Manowari mpya yenye uwezo wa kubeba silaha za nyuklia iliyozinduliwa na Korea Kaskazini juzi. **PICHA: REUTERS**

# Wanamgambo RSF walaani vikwazo

**KHARTOUM,** SUDAN

KIKOSI cha Wanajeshi wa dharula nchini Sudan (RSF), kimeshutumu vikwazo walivyowekewa na Marekani dhidi ya viongozi wake wawili, na kuvitaja kuwa si haki ni vya kushtua.

Juzi, Marekani iliweka vikwazo vya kifedha kwa naibu kiongozi wa RSF Abdel Rahim Dagalo na kupiga marufuku kusafiri kwa kamanda wa kundi hilo katika jimbo la Darfur Magharibi, Jenerali Abdul Rahman Juma, kwa madai ya ukiukaji wa haki za binadamu.

Dagalo na Jenerali Juma wamekanusha shutuma hizo na kusema ni za uongo na upotoshaji.

Katika taarifa iliyotolewa kwenye ukurasa wa X (zamani Twitter) juzi, RSF ilieleza vikwazo vya Marekani kuwa ni vya kushtua, vibaya na visivyo vya haki.

"Hazitasaidia kufikia moja ya malengo ya msingi ambayo yanapaswa kuzingatiwa, ambayo ni kutafuta suluhisho la kina la shida katika nchi yetu". Ilisema taarifa hiyo

Kundi hilo liliishutumu Marekani kwa kupuuza uhalifu wa kutisha unaofanywa na Jeshi la Sudan, ambalo lilisema ni pamoja na mashambulizi ya kiholela ya mabomu katika maeneo ya raia na mateso ya wanaharakati wanaopinga vita.

Kundi hilo la kijeshi lilisema vikwazo hivyo vitatatiza juhudi zinazoongozwa na Marekani za kuleta amani ya kudumu katika nchi hiyo.

Mwezi Juni, Marekani pia iliweka vikwazo kwa makampuni yanayomilikiwa na makundi yanayopigana. **BBC**

# Watu 64 wauawa kwenye mashambulizi

**BAMAKO,** MALI

WATU 64 wameuawa nchini Mali baada ya wanamgambo wa jihadi kufanya mashambulizi katika kambi ya kijeshi na boti ya abiria.

Mamlaka ya kijeshi nchini humo, zilisema kuwa shambulizi moja lililenga boti ya abiria katika mji wa Timbuktu katika Mto Niger na Linguine kwenye kambi ya kijeshi ya Bamba iliyoko katika Mkoa wa Kaskazini wa Gao na kuwaua raia 49 na askari 15.

Boti ya abiria ilikuwa ikipitia njia iliyoanzishwa kati ya miji mbalimbali kando ya mto na ilishambuliwa kwa roketi tatu zilizolenga injini zake.

Kundi moja lenye mafungamano na Al-qaeda lilidai kuhusika na mashambulizi yote mawili.

Serikali ya Mali imetangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa kuanzia jana.

Mto Niger ni kiungo muhimu cha usafiri katika maeneo ambayo hakuna miundombinu ya barabara. Kwenye tangazo la serikali, ilisema vikosi vyake vimewaua pia wapiganaji 50.

Tangu mwishoni mwa mwezi Agosti mwaka uliopita makundi yaliyo na silaha yamekuwa yakiuzuia mji wa Timbuktu baada ya jeshi la Mali kupeleka vikosi vyake katika eneo hilo.

Waasi wanazuia jiji hilo la jangwa kuingia bidhaa za muhimu.

Zaidi ya wakazi 30,000 wameukimbia mji huo na eneo jirani, kwa mujibu wa shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya kiutu. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KUPOTEA PASSPORT



**Hamis Kajala Kitela** mwenye picha hapo juu anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 407523** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Tarehe 11.5.2021. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:**RB/PHQ/SIM/ITI/235/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RIZIKI GOODLUCK CLEOPA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 364 DNG** aina ya **TOYOTA IST** yenye CHASSIS NO. **NCP610056911.** Engine namba **INZA903833.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/ARU/ARU/1462/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TWALBI OMARY NJIKITILE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 993 BZK.** Chassis namba **MD2B15BY7JWA912.** Engine namba **JVZWJA21051.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/2171/2023.**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMES MLAWA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 311 DKS - NISSAN XTRAIL.** CHASSIS NAMBA **NT30010490.** ENGINE NAMBA **QR20018421A.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. RB NO. **RUK/NKA/RB/140220/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALBINUS CHACHA IGOTI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 223 ABS.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/MAR/MUS/433/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JOSHUA STANLEY NGOWO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4981-0022** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ARUSHA CITY BOYS' SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/1861/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA TRECTOR

**KUWAYAWAYA STEPHEN KUWAYAWAYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari na trector, kadi ya gari aina ya Toyota Landcruiser yenye namba za usajili **T776AKK.** Chassis No. **HZJ800011044,** Engine No. **IHZ006063.** Kadi ya trector yenye namba za usajili **T 532 BXP.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/RB/2232/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI

**ROMAN CATHOLIC DAYOSISI YA GEITA,** inatangaza kupotea kwa Cheti cha Usajili chenye namba **SO.NO.10476,** Kilichotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Msajili wa Jumuiya, Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **REF/GE/TR/RB/1703/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **DOMITILA DOMI MATABU** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T785 BMK.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/191251/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

---

**FOMU MIRATHI-2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa Dar es salaam**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1348/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NEEMA SAID KIMEZA WA KONDOA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FATUMA JUMA RAJABU**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 mwezi 10 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetokewa leo tarehe 07 mwezi 09 mwaka 2023

HAKIMU

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP.117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

BY THIS DEED I **IBRAHIM TAMIM KAVENUKE** of Iringa do hereby ABSOLUTELY and renounce ,relinquish and abandon the use name of **IBRAHIM MAGELASA KAVENUKE** which appeared in **NIDA CARD NO 19850424514090000129** And in lieu thereof do assume the name **IBRAHIM TAMIM KAVENUKE** which appeared in BIRTH CERTIFICATE.
For the purpose of such determination, I hereby **DECLARE** that he shall at all times here in after in all records,deed,documents and other writings and in all actions, suits and proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and creations.
Whatsoever use and subscribe the said name of **IBRAHIM TAMIM KAVENUKE** in lieu of and in substitution of former name of **IBRAHIM MAGELASA KAVENUKE.**
When I registered,I used the name of Ibrahim Magelasa Kavenuke ,which is my grandfather's name, and on the birth certificate Iused the name of Ibrahim Tamim Kavenuke, which is my father's name ,so I want to remain my name of Ibrahim Tamim Kavenuke.
**AND I DO HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated,describe and address him by the adopted name of **IBRAHIM TAMIM KAVENUKE**
**IN WITNESS WHERE OF** I have set my hands at Iringa,and **I HERE BY** substitute the name
of IBRAHIM MAGELASA by the new name of **IBRAHIM TAMIM KAVENUKE** of.

SIGNED and DELIVERED by the said
IBRAHIM TAMIM KAVENUKE
Who is known to me personally/identified
To me by ..............................
The latter being known to me personally
In my presence this .....05.....
Day of ............................ SEPTEMBER, 2023
BEFORE ME:
Name: HASSAN MLATLA
Signature ..........
Postal address: ...
Qualification RESIDENT MAGISTRATE IRINGA

DEPONENT



---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 87 LA 2021**

**JOHN KENGERE BOGOMBA................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **SOPHIA KAONEKA**
2. **SELEMAN KAONEKA**
3. **KILUA KAONEKA**
4. **MAJEMBE AUCTION MART LTD..........MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **SOPHIA KAONEKA**
2. **SELEMAN KAONEKA**
3. **KILUA KAONEKA**
4. **MAJEMBE KAONEKA..........PO POTE ULIPO/MLIPO**

**JOHN KENGERE BOGOMBA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyuma lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 19/9/2023 saa 03:00 asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaarifiwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 03 Mwezi wa 08/2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

**MAHAKAMA YA MWANZO MVOMERO WILAYA YA MVOMERO**

**MADAI NAMBARI 27/....2023**

**MDAI: MARTHA SELEMANI LYANGA**
**ANAMDAI**
**MDAIWA: JULIASI ELIASI**

**KWA: JULIASI ELIASI**
**WA POPOTE ULIPO**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:UNAHITAJIKA KUJA KUJIBU DAI LA TALAKA NA MGAO WA MALI DHIDI YAKO .**

Kwa hiyo nahitajiwa/mnahitajiwa Kuhuduria binafsi katika Mahakama hii siku ya jumatatu tarehe 11/09/2023 saa 03:00 asubuhi kwa mjibu wa Madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinahusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. ANGALIZO:Kama hukudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shauri hili,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa Amri na yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 07/09/2023.

Futa lisilotakiwa*
FAHAMU:
Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 82 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the Late: MESHACK BUHANZA HUTA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION**

**By 1. GEVAMEN MESHACK HUTA**
**2. .....................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 14 day of 09..2023

Dated at Morogoro this 04 day of September..2023

Resident Magistrate
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE INCHARGE
DISTRICT COURT
P.O. Box 660, Morogoro

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KatikaMahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU**

**Shauri la madai/Ndoa Na 33/2023**

**Jina la Mdai: ALPHONCE APOLINARI BONIPHACE**

**Jina la Mdaiwa: ELIZABETH MARCO BUSIGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:ELIZABETH MARCO BUSIGA**
**WA DAR ES SALAAM**

Kwa kuwaMdai ameleta madai yake YA TALAKA
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 14 Mwezi 09 Mwaka 2023 saa2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini.Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 24 Mwezi 08 Mwaka 2023

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE GEITA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBINGA**

**MBINGA**

**SHAURI LA MAOMBI YA UTEKELEZAJI NO. 3/2023**

**(Lililotokana na Shauri la Madai Na. 12/2022 Mahakama ya Wilaya Mbinga)**

**KATI YA**

**AMSEK SECURITY SERVICE LIMITED..................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**CHINA HENAN INTERNATIONAL CO OPERATION GROUP COMPANY LIMITED (CHICO LTD)......................MJIBU MAOMBI**

**KWA: CHICO LTD.**

Unaamuriwa kufika Mahakamani tarehe **14/09/2023** saa mbili na nusu asubuhi siku ambayo shauri la maombi ya utekelezaji tajwa hapo juu limepangwa kwaajili ya kutajwa.

Imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe **31/08/2023.**

**A.A. MKAMA**
**HAKIMU MKAZI MKUU**
**MAHAKAMA YA WILAYA MBINGA**

HAKIMU MKAZI WILAYA MBINGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NA. 61 YA MWAKA 2023**

**KELVIN SEBASTIAN MSOLA ........................................MDAI**

**DHIDI YA**

**IMARISHA MAISHA FINANCIAL SERVICES LIMITED ............MDAIWA**
**KIBAIGWA AUCTION MART AND COMPANY LIMITED.......... MDAIWA**
**SIGHMAN SAFARI HAULAGE LIMITED................................MDAIWA**

**KWA:**
**KIBAIGWA AUCTION MART AND COMPANY LIMITED**
**POPOTE WALIPO.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya hati madai ambayo inapatikana katika Mahakama hii, Kwa hiyo unaamriwa kuhudhuria katika mahakama hii wewe binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 12/09/2023 saa 3:00 Asubuhi Mbele ya Mhe. A.H. MSUMI PRM.

**ANGALIZO:** kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, inaweza kutoa Hukumu dhidi yako kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 28 ya mwezi AUGUST, 2023.

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU -DAR ES SALAAM
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

Alinipigia simu kuwa leo atakuwa hapa tuonane, na akasema atakuwa na shemeji yake, lakini wakati mimi nimeshafika Mwenge kituoni akaniambia amepatwa tatizo na hatofika. Nikamwambia mimi niko hatua kadhaa kabla ya kufika kwenye baa hii, akaniambia basi kama hivyo nimtafute shemeji yake anaitwa Nancy na nimkirimu kila atakachotaka kama vile ambavyo alitaka kufanya wakati yeye yupo.

# Maiti kwenye kiroba-**25**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

***Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani ndio wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Wakinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.***

****************************************




Alichogundua Eddy ni kwamba Nancy ana vitu vingi kifuani ambavyo vinaweza kumfanya apate kitu kingine ambacho hajakijua kwenye kesi hii.

Ana uhakika kuwa Charton ndiye aliyemuua mkewe akishirikiana na Tinga, hivyo kwa hili akawa anajiuliza Rukia naye kamuua nani?

“Kwani shemeji upo wapi saa hizi?”

“Nipo kwetu Boko.”

“Basi tunaweza kuonana jioni?”

“Wapi, maana unanijua mimi, sikai sehemu bila mbili baridi.”

Ndipo Eddy alipogudua kuwa Nancy ni mnywaji, hivyo ilikuwa rahisi tu kwake kumbia akodishe bajaj mpaka Mwenge na kama atawahi kabla yake afike kwenye baa iliyo nyuma ya majengo ya TRA na kuagiza kinywaji yeye atafika baadaye.

“Basi shemeji kwanza nirushie hiyo pesa ya bajaj maana hapa sina hata mbuni.”

“Nakutumia elfu ishirini, na kama nitachelewa anza kunywa.”

“He, shemeji leo naona umejaa, ndiyo maana umebadilisha hata namba ya simu.”

“Usijali hata kama mmegombana na Charton, lakini wewe ni shemeji yangu tu, lakini nikupige ofa,” akadanganya.

Tayari kuna kitu ameshaona huenda kwenye mauaji ya Tessy pia kuna kitu kingine nyuma ya pazia.

******************************

Alifika kwenye baa moja nyuma ya jengo la TRA maeneo ya Mwenge Dar es Salaam. Gari lake alilisimamisha mbali. Ilikuwa ni nje ya soko la Mwenge, kando ya barabara.

Alitembea taratibu mpaka akafika. Aliingia taratibu na alichofanya kwanza moja kwa moja alielekea maliwatoni.

Nia haikuwa kujisaidia lakini ni kutaka kutambua anayemfuata ni nani na amekaa wapi.

Kati yao hakuna aliyekuwa anamtambua mwenzake. Hakutaka kuanza kuonekana na anayemfuata kabla ya yeye kumuona.

Hii ni kanuni ya wapelelezi wote. Ni kwamba yoyote anayemfuata au kuahidiana kuonana yeye ndiye anataka awe kwa kwanza kumuona. Yupo wapi, amekaa vipi, wapi, anafanya nini na hapo ndipo atamua iwe vipi, kumfuata au kuahirisha.

Kanuni hii huwasaidia sana kuepuka mipango miovu juu yao, au mikakati ya kutaka kuwadhuru au kuwaua.

Na mara nyingi huwa hawafiki muda ambao wameahidiana kukutana.

Mpelelezi yoyote hata kama jambo la kawaida tu, atawahi eneo la kukutania bila mwenzake kujua ili kuangalia kama kuna mpango wowote mbaya, au atachelewa ili kuivuruga tu mipango ya waandaaji.

Baada ya kujifanya amejisadia alianza kupiga simu yake huku akitoka. Alipofika mlangoni akaanza kuangalia ni wapi ambapo kuna mtu anasikiliza simu.

Kwa mbali alimuona dada mmoja aliyekuwa amekaa peke yake akipokea simu. Halafu akasikia sauti, “vipi shemeji uko wapi, mimi nimeshafika.”

Eddy hakujibu chochote, akaikata simu. Tayari alishajua anayemfuata yu wapi.

Aliizipapasa silaha zake akaona zipo kwenye hali nzuri na sehemu aliyohitaji kwa ajili ya kuitumia haraka kwa chochote kitakachotokea.

“Usimumini mtu yoyote au kitu chochote hata kama ni maiti.” Akakumbuka kanuni hiyo.

Akaelekea moja kwa moja mpaka kwa mwanadada huyo ambaye alikuwa na uhakika kuwa atamshangaa.

“Hujambo Nancy?” Akasalimia akitabasamu, huku uso wa mwanadda huyo ukiwa na mshangao.

Alitarajia kuonana na Chimozi, rafiki ya mpenzi wake Charton ambaye anadai wameachana.

“Najua unashangaa kutomuona Chomozi. Chimozi ni rafiki ya mpenzi wako Charton, lakini ujue pia kuwa naye ana rafiki zake ambaye ni mimi. Yeye amepatwa na udhuru, hatokuja tena hapa.”

Bado uso wa Nancy ulionekana kuwa na mshangao uliochanganyikana hasira pia.

“Alinipigia simu kuwa leo atakuwa hapa tuonane, na akasema atakuwa na shemeji yake, lakini wakati mimi nimeshafika Mwenge kituoni akaniambia amepatwa tatizo na hatofika. Nikamwambia mimi niko hatua kadhaa kabla ya kufika kwenye baa hii, akaniambia basi kama hivyo nimtafute shemeji yake anaitwa Nancy na nimkirimu kila atakachotaka kama vile ambavyo alitaka kufanya wakati yeye yupo.”

Nancy akawa kama na mashaka, akachukua simu yake na kupiga. Wakati Eddy akijiandaa na uongo mwingine iwapo Chimozi atapatikana, simu ilikuwa inaita kwa muda mrefu lakini haikupokelewa. Alifanya hivyo kama mara tatu kashusha pumzi.

> **Nancy akawa kama na mashaka, akachukua simu yake na kupiga. Wakati Eddy akijiandaa na uongo mwingine iwapo Chimozi atapatikana, simu ilikuwa inaita kwa muda mrefu lakini haikupokelewa. Alifanya hivyo kama mara tatu kashusha pumzi.**

“Ana tatizo gani?” Hatimaye Nancy alivunja ukimya.

“Hata mimi hakuniambia, inawezekana ana tatizo la kifamilia au la kibinafsi ambalo hataki watu wajue.” Bado Eddy aliendelea kumuongopea.

“Mpaka sasa umekunywa bia ngapi?” Akauliza kwa lengo la kumfanya ampotezee Chimozi na akili arudi kwake.

“Hii ya pili sasa.” Akajibu kivivuvivu.

“Unaweza kuongeza nyingine mbili kama utataka. Kwanza umekula mrembo?”

“Mh! Ndiyo nilikuwa namsubiri shemeji hivyo nimwambie.

Nimeanza na hizi mbili, halafu nile kwanza.”

Eddy alimwita mhudumu na kumwambia amsikilize kwanza Nancy.

“Niletee chips, kuku nusu na maji kubwa.” Akaagiza.

Eddy alijipigia makofi kimoyomoyo. Alijua kabisa dakika 10 tu baada ya hapo, mwanadada huyu hatomkumbuka tena Chimozi.

Pamoja na kuwa ni mpelelezi wa kiwango cha juu Afrika, lakini pia alikuwa mtaalam kwenye masuala ya kijamii hasa mambo yanayohusu mahusiano na mapenzi.

Moja ya kitu ambacho alicho na uzoefu nacho ni kwamba ni vigumu sana kumshawishi mwanamke kwa njia yoyote ile kama hakupi nafasi ya kukusikiliza.

Mwanamke akikataa kumpa nafasi mwanaume basi huwezi kufanya chochote kile. Lakini kama atatoa nafasi, basi kwa wanaume kwenye sanaa ya kushawishi anakuwa amekwisha.

Eddy ni mmoja wa wanaume ambao wana uwezo mkubwa wa kuongea na kushawishi.

Kitendo cha kumsikiliza na kuanza kuagiza chakula, alikuwa ameshamaliza kila kitu.

“Na mimi niletee ndizi mbili za kuchoma, mishikaki minne na juisi ya embe kama ipo.” Eddy naye aliagiza.

Eddy alichokuwa akihitaji ni kupata siri nyingi za Charton aliyemuua mkewe Tessy. Na kwa sababu walikuwa wameachana kama alivyodai Nancy na kuonekana kulalama kuachwa na kuchukuliwa Rukia alijua atazipata tu.

Hata hivyo moja kati ya vitu anavyotakiwa kuvifanya ili azipate kwa urahisi zaidi si kwa kujifanya polisi au mpelelezi. Urafiki pekee ndiyo utamfanya kuua tembo kwa ubua. Ni kutengeneza urafiki wa kimapenzi japo wa muda. Alijua hiki ni kipindi ambacho Nancy ana maumivu ya kuachwa na Charton, hivyo ingekuwa rahisi kumshawishi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KOCHA MPYA SINGIDA FG AWAPIGIA HESABU FUTURE

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu mpya wa Singida Fountain Gate FC, Ernest Middendorp, ameanza kufanyia kazi ubora wa wapinzani wao katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Future FC kutoka Misri, imefahamika.

**Singida Fountain Gate ambayo ipo Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa hatua ya kwanza utakaochezwa Septemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex.**

Ofisa Habari wa timu hiyo, Hussein Masanza, aliliambia gazeti hili Kocha Middendorp ameshaanza kazi na anaonekana zaidi anawajenga viungo ili kuwaweka tayari kuwakabili Waarabu hao kutokana na uwezo waliokuwa nao.

Masanza alisema kocha huyo anaamini muda uliopo utamsaidia kukiimarisha kikosi chake huku tayari ameshafahamu baadhi ya nyota tegemeo wanaotakiwa kuchungwa katika kikosi cha Future akiwamo, Ahmed Refaat, ambaye anaweza kucheza winga zote mbili na kiungo mshambuliaji.

Alisema baada ya benchi la kufatilia video za michezo mbalimbali ya kimataifa walizocheza hivi karibuni, wamebaini wachezaji sita waliokuwa hatari wameondoka katika timu hiyo.

"Kocha amefanikiwa kuwafuatilia Future na kuona ubora wao, amewajua baadhi ya wachezaji ambao ni roho ya timu, wako imara kwenye safu ya kiungo (Refaat) ambaye amekuwa akisumbua sana kwenye mechi zilizopita," alisema Masanza.

Aliongeza wanaendelea kufanyia kazi mapungufu ya timu yao yaliyojitokeza katika mechi zilizopita ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Future FC ni wazuri, tunajiandaa vyema kuwakabili kwa sababu tutaingia uwanjani kama 'under dog', tunawaheshimu wapinzani wetu kulingana na ubora waliokuwa nao," Masanza alisema.

Kuelekea mchezo huo wa kimataifa, kikosi chake kinatarajia kujiimarisha kwa kucheza mechi mbili ngumu za kirafiki na huenda leo ikavaana na Maafande wa JKT Tanzania.






Meneja Mkuu wa Kampuni ya Betika, Alec Wehbe (kushoto), akimkabidhi funguo ya mfano mshindi wa shindano la kurusha kindege wa Aviator, Anselim Mangu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Mkunga ashinda daladala la Aviator*

**Mwandishi Wetu**

MKUNGA na muuguzi, Anselim Mangu, ameshinda zawadi ya gari aina ya Nissan Civillian katika mchezo wa kurusha kindege wa Aviator unaosimamiwa na Kampuni ya Betika.

Mangu ambaye ni mkazi wa Chemba, Dodoma amekabidhiwa gari hiyo jana katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam, akipiga hesabu ya kuitumia kufanya safari kutoka Dodoma kwenda Kondoa.

Akizungumzia ushindi huo Mangu alisema, alianza kucheza katikati ya Agosti baada ya kusikia tangazo.

"Niliweka Sh. 30,000, nikashinda 500,000, sikuitoa yote, nikaendelea kucheza hadi napigiwa simu nimeshinda, nilitumia kama 800,000," alisema mshindi huyo.

Aliongeza ushindi huo umempa mwanga mpya katika maisha yake na sasa amepanga kwenda kupata fursa nyingine ya kipato kwenye usafirishaji wa abiria.

Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa, alisema mchezo wa Aviator ulianza mapema Agosti na utamalizika mwishoni mwezi huu na kauli mbiu yake ni Mbegu Zimefunguka.

Rugambwa alisema mbali na zawadi kubwa ya kila mwezi ya Daladala, pia kuna washindi watano wa kila siku ambao kila mmoja anajipatia Sh. 500,000.

## Kuogelea vijana wang'ara Israel

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya taifa ya vijana ya kuogelea imeendelea kufanya vyema katika mashindano ya dunia yanayoendelea nchini Israel kwa kufanikiwa kuvunja rekodi ya muda, imethibitishwa.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alexander Mwaipasi, alisema wachezaji wengi wamefanikiwa kupunguza muda na kwa maana hiyo wamevunja rekodi zilizokuwa zimewekwa na wachezaji waliopita wa Tanzania katika mchezo huo.

Mwaipasi alisema tangu michuano hiyo ilipoanza mapema wiki hii, wachezaji wake wameonyesha uwezo mkubwa licha ya kuwapo na upinzani mkubwa.

"Tangu mashindano haya yaanze timu yetu imefanya vizuri kwa wastani, vijana wamefanikiwa kupunguza muda, ikiwa pamoja na kuvunja rekodi ya matukio ambayo hatujawahi kuyafanya, tunaomba Watanzania waendelee kutuombea," alisema Mwaipasi.

Wachezaji hao wa Tanzania jana asubuhi wanaume walichuana katika umbali wa mita 100 kwa mtindo wa Free style wakati wanawake walishiriki katika umbali wa mita 50.



## KMKM, JKU kusaka Ngao ya Jamii Z'bar leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIKOSI cha KMKM kinatarajia kukutana na JKU katika mechi ya kuwania Ngao ya Jamii ya Zanzibar (ZFF FA Cup), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mao ze Dong.

Mchezo huo ni ishara ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo itaanza rasmi Septemba 13, mwaka huu kwenye viwanja mbalimbali.

Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, aliliambia gazeti hili timu yake imejiaandaa vyema na wamejipanga imara kuhakikisha wanashinda mchezo huo ili kuwa na mwanzo mzuri wa ligi.

"Tumefanya maandalizi mazuri, wachezaji wote wamehamasika katika kuhakikisha tunashinda mchezo huo, najua tunaenda kucheza na timu ngumu ambayo inauzoefu katika Ligi ya Zanzibar, tutakuwa makini katika uchezaji wetu,"alisema Msimu.

Naye Kocha wa JKU, Salum Ali, alisema mchezo huo utakuwa mgumu tofauti na unavyoangaliwa na mashabiki wa soka visiwani hapa lakini anaamini dakika 90 ndio zitaamua nani ni bora.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WALIMTAKA SANCHO

WINGA wa Manchester United, Jadon Sancho, alikuwa akilengwa na Al-Ettifaq kabla ya dirisha la Ligi Kuu ya Saudia kufungwa Alhamisi walipokuwa wakijaribu kumsajili kwa mkopo mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 23. ***(CBS Sports)***

### POTTER AIKATAA LYON

KOCHA wazamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter, 48, amekataa kuchukua nafasi ya Laurent Blanc katika klabu ya Lyon ya Ufaransa. ***(90 min)***

### ROONEY ANUKIA BIRMINGHAM

MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Wayne Rooney mwenye umri wa miaka 37, anaweza kuichukua Birmingham City ikiwa kocha wa sasa, John Eustace, ambaye amekuwa akihusishwa na Swansea na Rangers, ataondoka katika klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### PEPE ATAKIWA UTURUKI

ARSENAL ina tumaini inaweza kufikia makubaliano ya uhamisho wa winga wa Ivory Coast, Nicolas Pepe, kuhamia Uturuki, huku Besiktas na Trabzonspor zikisemekana kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Evening Standard)***

### NUSA AGEUKA LULU ULAYA

CHELSEA ilikuwa na ofa ya pauni milioni 23 kwa winga wa Norway, Antonio Nusa, iliyokataliwa na Club Brugge siku ya mwisho ya uhamisho na itakabiliwa na ushindani mkubwa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 katika siku zijazo huku akitazamwa na angalau klabu zingine 20. ***(Evening Standard)***

### LINGARD NA WEST HAM

KIUNGO mshambuliaji wa England, Jesse Lingard, 30, alitazamiwa kuichezea West Ham katika mechi ya kirafiki ya bila mashabiki dhidi ya Ipswich, huku wagonga nyundo hao wakifikiria kumpa mkataba mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United. ***(Mail)***

### ‘KVARATSKHELIA HAONDOKI’

WAKALA wa winga wa Napoli, Kvicha Kvaratskhelia, 22, amesema mchezaji huyo wa kimataifa wa Georgia anaridhika katika kikosi cha Serie A na “hatukuwahi kuzungumza kuhusu kutaka kubadilisha klabu”. ***(CalcioNapoli24, kupitia Football Italia)***

### REED, FULHAM KUJADILIANA

KLABU ya Fulham inajadiliana na kiungo wa kati wa England, Harrison Reed, 28, kuhusu mkataba mpya, huku wakiwa wamekataa dau la pauni milioni tatu kutoka kwa Wolves kwa ajili ya mchezaji huyo wakati wa dirisha la uhamisho. ***(Evening Standard)***

### KELLY KUINGIA SOKONI

KLABU ya Bournemouth ilikataa dau la mwisho la pauni milioni 20 kwa mlinzi wa England, Lloyd Kelly, 24, msimu wa joto na Tottenham Hotspur wanaweza kuunganishwa na Liverpool na Newcastle United kutaka kumsajili mchezaji huyo katika dirisha la Januari. ***(90 min)***

### FERGUSON ANUKIA CITY

KWA mujibu wa Inews, Manchester City inamtaka mshambuliaji wa Brighton & Hove Albion, Evan Ferguson. Huenda Januari ikapeleka ofa kwa klabu yake. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR AJITETEA KUITWA BRAZIL

**SAO PAULO,** Brazil

**●●● Mshambuliaji huyo asema hajakuwa fiti kwa asilimia 100 ili...**

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar amesema hayuko sawa kabisa kucheza katika mechi mbili za kwanza za kufuzu fainali zijazo za Kombe la Dunia kutokana na jeraha la kifundo cha mguu wa kulia ambalo limemweka nje tangu Februari, mwaka huu.

**Neymar aliondoka Paris Saint-Germain na kwenda Al-Hilal ya Saudi Arabia lakini bado hajaichezea klabu yake hiyo mpya.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Neymar alisema Ligi Kuu ya Saudia inaweza kuwa bora kama Ligue 1 ya Ufaransa.

Jana Brazil ilicheza mechi yake ya kwanza katika safari ya kufuzu Kombe la Dunia 2026 katika mji wa Amazon wa Belem dhidi ya Bolivia na wataondoka kuifuata Peru ambayo watavaana nayo hapo Jumanne.

Neymar alifafanua hali yake ya jeraha kabla ya mechi hizo baada ya Kocha wa Al-Hilal, Jorge Jesus, kulikosoa Shirikisho la Soka la Brazil (CBF) kwa kumwita akiwa bado hana hali ya kucheza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alisema amejiunga na Brazil katika hali kama hiyo hapo awali na bado alicheza.

“Ninajisikia vizuri, mwenye furaha, lakini ni wazi siko fiti kwa asilimia 100%. Lakini kichwa changu kipo vizuri, mwili wangu uko vizuri,” alisema Neymar.

“Nilikuwa naenda kucheza mechi ya hivi karibuni zaidi ya Al Hilal, lakini kocha alichagua kuniacha nje, ili nije Brazil.”

Mechi ya mwisho zaidi ya Neymar akiwa na Brazil ilikuwa ni kupoteza dhidi ya Croatia katika hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia. Aliondoka Qatar akiwa na shaka kuhusu mustakabali wake katika timu ya taifa na hakucheza mechi tatu za kwanza za Selecao mwaka huu.

“Baada ya shinikizo kubwa kutoka kwa familia na marafiki kurejea kwenye timu ya taifa unaanza kutoa thamani kwa kila ulichofanya,” aliongeza Neymar.

“Unapokuwa na watu wako, familia yako, wanakuweka kwenye nafasi yako na kukufanya uone inafaa kuendelea kuwa na furaha kwa kuvaa jezi ya Brazil.”

Neymar anahitaji bao moja ili kuipiku rekodi ya mabao 77 ya Pele kama mfungaji bora wa Brazil kwa wakati wote.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,151,10

MECHI KALI

UKRAINE
VERSUS
ENGLAND

1 | 7.12
X | 4.16
2 | 1.47

tigo pesa SportPesa

WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!

1. Asma Mwasisime - 0653 623 XXX
2. Lunyama Sabato - 0658 320 XXX
3. Gabriel Mshana - 0658 523 XXX
4. Fedrick Tengula - 0672 178 XXX
5. Tatu Hassan - 0673 131 XXX
6. Amina Jumanne - 0675 339 XXX
7. Albert Mosha - 0676 622 XXX
8. Daniel Mbembele - 0710 264 XXX
9. Gadson Godson - 0713 583 XXX
10. Elly Chunga - 0717 243 XXX

20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SANCHO MAMBO MAGUMU UNITED




**MANCHESTER,** England

JADON Sancho anakabiliwa na vita ya kurejesha uungwaji mkono kutoka kwa wachezaji wenzake wa Manchester United pamoja na Kocha, Erik ten Hag baada ya hasira yake ya kuachwa kwenye kipigo cha Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal, chanzo kimeiambia ESPN.

Sancho (23), alichapisha maneno makali kwenye mtandao wa kijamii akipinga madai ya Ten Hag baada ya kumalizika kwa mechi hiyo akidai aliondolewa kwenye kikosi kutokana na mazoezi yasiyoridhisha, huku mchezaji huyo akikataa maoni hayo "yasiyo ya kweli" na kusema kupitia X alifanywa 'mbuzi wa kafara'.

Lakini chanzo kimoja kiliiambia ESPN kuna huruma kidogo kwa Sancho ndani ya chumba cha kubadilishia nguo cha United, kikisema, "Wachezaji wenzake wamemchoka."

Uchezaji wa Sancho mazoezini na siku ya mechi, pamoja na mwenendo wake katika klabu hiyo, umesababisha usajili wa pauni milioni 73 kutoka Borussia Dortmund kutokuwa na manufaa.

Licha ya majibu ya haraka ya Sancho kwa maoni ya Ten Hag kwenye mkutano wa waandishi wa habari baada ya mechi dhidi ya Arsenal -- Sancho hajafuta kauli hiyo.




## Mo Salah abakia Liverpool

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah atabakia Liverpool kwa siku za usoni baada ya dirisha la usajili la Ligi ya Saudi Arabia kufungwa rasmi juzi.

Wiki iliyopita, ESPN iliripoti Liverpool ilikataa ofa yenye thamani ya hadi pauni milioni 150 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri kutoka kwa Al-Ittihad.

Iliripotiwa klabu hiyo ya Saudia ingejaribu kutoa ofa ya juu zaidi kwa ajili ya Salah katika siku yao ya mwisho ya uhamisho lakini hilo lilishindikana.

Katika kipindi chote cha uhamisho wa wachezaji, Liverpool wamekuwa wakisisitiza Salah hataruhusiwa kuondoka Anfield baada ya wachezaji wa zamani Jordan Henderson, Sadio Mané, Fabinho na Roberto Firmino kutua katika klabu za Saudia.

Baada ya Salah kufunga katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Aston Villa Jumapili iliyopita, Kocha, Jurgen Klopp alisisitiza msimamo wa klabu hiyo na kusema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amejitolea kikamilifu katika timu hiyo.

04,636/-

# SIMBA SC KUIFUATA DYNAMOS ALHAMISI, AKRAMO MTEGONI

**Na Saada Akida**

MABINGWA wa Ngao ya Jamii, Simba wanatarajia kuondoka nchini Septemba 14, mwaka huu ili kuelekea Zambia kwa ajili ya mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji, Power Dynamos, imefahamika.

Power Dynamos itawakaribisha Simba katika mechi ya kwanza ya hatua ya kwanza ya michuano hiyo itakayochezwa Septemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko katika mji wa Ndola.

**Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha timu hiyo kinaendelea vyema na mazoezi na wachezaji wataingia kambini rasmi leo ili kuongeza umakini.**

Ahmed alisema wanataka kuona kila mchezaji anakuwa imara na tayari kwa ajili ya mechi hiyo muhimu.

Alisema wachezaji wote wako vizuri na tayari Kocha Mkuu, Roberto Oliviera 'Robertinho', ametoa majukumu 'mazito' kwa wachezaji wake baadhi akiwamo winga machachari, Aubin Kramo.

"Wachezaji wote wapo sawa na wanaendelea vizuri na programu zangu isipokuwa kwa wale ambao wapo katika majukumu ya timu zao za taifa, tumepata muda mrefu wa kukamilisha mambo ya msingi kuelekea katika mchezo wetu wa Zambia, kitu kizuri tunaenda kucheza na mpinzani tunayemfahamu vyema, hatuhitaji kupuuzia kwa sababu tunawafahamu.

Matarajio yetu ni kuongeza nguvu kubwa katika mazoezi kutokana na majukumu ambayo kila mchezaji tumempatia ili kufikia malengo," alisema Ahmed.

Simba iliwaalika Power Dynamos katika Tamasha la Simba Day na katika mchezo huo wa kirafiki wa kimataifa wenyeji walipata ushindi wa mabao 2-0.



Kipa wa zamani wa Taifa Stars, Simba na Yanga, Juma Kaseja (kushoto), akimweleza jambo mwanafunzi mwenzake, Stephen Marashi, anayeshiriki Kozi ya CAF A Diploma inayoendelea jijini, Tanga. **PICHA: TFF**

## Pacome kuipeleka Yanga makundi CAF

ENDELEA UKURASA 23

makali ya wiki mbili.

"Ninaamini kwa asilimia 80 nyota wangu wameimarika, ninahitaji kikosi bora ambacho kitatoa ushindani katika kila mchezo. Mechi zote tunazocheza zina ushindani, hatudharau timu, tunataka kupambana ili kufikia malengo, lazima tujiimarishe," aliongeza Gamondi.

Katika kuwajenga nyota wake, wiki hii Gamondi alikiongoza kikosi chake katika mazoezi ya ufukweni ili kuwatengenezea pumzi wakati juzi na jana walihamia katika mazoezi ya gym (asubuhi) na jioni walihamia uwanjani.

Yanga ndio mabingwa watetezi na vinara katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itaendelea tena kuanzia Septemba 15, mwaka huu baada ya kupisha kalenda ya kimataifa kumalizika.

## Stars walamba 500m

ENDELEA UKURASA 23

nayo ambayo ni kufuzu.

"Wamepambana sana, wamecheza kwa fiziki kubwa, mpango mkakati haukuwa rahisi kupata hata sare, tulicheza na timu kubwa yenye wachezaji wakubwa ndiyo maana tuliamua kucheza tulivyocheza kwa ajili ya kufanikisha malengo, ni fahari kwa taifa la Tanzania, nawapongeza wachezaji, benchi langu la ufundi, serikali, TFF na wote waliofanikiwa kufika hapa, tunachoangalia sasa ni jinsi gani tutakwenda kupambana huko mbele," alisema kocha huyo ambaye ana uraia pacha wa Algeria na Ubelgiji.

Nafasi ya tatu katika Kundi F ilishikwa na majirani Uganda (Uganda Cranes) iliyomaliza ikiwa na pointi saba na Niger iliyoburuza mkia kwa pointi mbili.

Kwa mara ya kwanza tangu nchi ipate Uhuru, Tanzania ilitinga fainali hizo mwaka 1979 ilipoitoa Zambia na kucheza fainali zake zilizochezwa mwaka uliofuatia huko Nigeria na mara ya pili iliwa ni mwaka 2019 ilipowafunga Uganda mabao 3-0 na kucheza AFCON zilizofanyika Misri.


# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.09/09/23 | 17:00 | AFC Wimbledon vs Stockport County FC | 2.75 | 3.20 | 2.47 |
| 02.09/09/23 | 17:00 | Milton Keynes Dons vs Notts County | 2.60 | 3.55 | 2.41 |
| 03.09/09/23 | 17:00 | Accrington Stanley vs Mansfield Town | 2.95 | 3.40 | 2.24 |
| 04.09/09/23 | 17:00 | Crawley Town vs Newport County | 3.00 | 3.30 | 2.25 |
| 05.09/09/23 | 17:15 | Burgos CF vs SD Eibar | 2.80 | 2.90 | 2.65 |
| 06.09/09/23 | 19:30 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.25 | 2.90 | 3.40 |
| 07.09/09/23 | 20:45 | Cobh Ramblers vs Athlone Town AFC | 2.36 | 3.40 | 2.48 |
| 08.09/09/23 | 22:30 | Virgin Islands, British vs Turks and Caicos Islands | 2.44 | 3.30 | 2.45 |
| 09.10/09/23 | 00:00 | Cerro Largo FC vs CA Fenix Montevideo | 2.46 | 3.00 | 2.60 |
| 10.10/09/23 | 03:30 | FC Tulsa vs Phoenix Rising FC | 2.41 | 3.25 | 2.50 |
| 11.10/09/23 | 04:00 | Colorado Springs Switchbacks FC vs San Antonio FC | 2.60 | 3.25 | 2.34 |
| 12.10/09/23 | 05:30 | Portland Timbers vs Los Angeles FC | 2.65 | 3.50 | 2.19 |
| 13.10/09/23 | 14:30 | Shanghai Jiading City Dev vs Heilongjiang Ice City | 2.60 | 3.15 | 2.40 |
| 14.10/09/23 | 16:00 | Kazakhstan vs Northern Ireland | 2.55 | 2.90 | 2.60 |
| 15.10/09/23 | 16:00 | CA Cerro vs CA River Plate (URU) | 2.42 | 2.95 | 2.70 |
| 16.10/09/23 | 19:00 | Faroe Islands vs Moldova | 2.80 | 2.90 | 2.40 |
| 17.10/09/23 | 21:00 | Tristan Suarez vs Deportivo Riestra | 2.75 | 3.00 | 2.60 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 09/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 3484 | China vs Malaysia | 1.48 | 4.41 | 6.31 |
| 16:00 | 1677 | Azerbaijan vs Belgium | 11.35 | 5.48 | 1.27 |
| 16:00 | 2403 | Malawi vs Guinea | 2.74 | 3.10 | 2.55 |
| 16:00 | 4037 | Mozambique vs Benin | 2.10 | 3.05 | 3.62 |
| 16:00 | 5263 | South Africa vs Namibia | 1.59 | 3.84 | 5.89 |
| 16:30 | 4416 | Penybont vs Colwyn Bay | 1.45 | 4.04 | 5.86 |
| 16:30 | 5422 | Aberystwyth Town vs Caernarfon Town | 3.24 | 3.34 | 1.99 |
| 16:30 | 5750 | Barry Town FC vs Gap Connahs Quay | 4.14 | 3.68 | 1.68 |
| 17:00 | 2317 | Dungannon Swifts vs Glenavon | 2.78 | 3.43 | 2.18 |
| 17:00 | 4502 | Carrick Rangers vs Ballymena Utd | 1.98 | 3.44 | 3.18 |
| 17:00 | 4862 | Rapperswil vs Breitenrain | 1.67 | 3.94 | 3.89 |
| 17:00 | 5467 | Stevenage vs Carlisle | 1.73 | 3.56 | 4.51 |
| 17:00 | 5977 | Start Brno vs Uhersky Brod | 1.54 | 4.17 | 4.78 |
| 17:15 | 1668 | Burgos vs Eibar | 2.93 | 2.88 | 2.49 |
| 17:30 | 1202 | NK Bilje vs PSC Tolmin | 1.60 | 3.78 | 4.53 |
| 17:30 | 1770 | Indjija vs FK Graficar Beograd | 2.00 | 3.27 | 3.27 |
| 17:30 | 2867 | NK Nafta vs Tabor Sezana | 1.36 | 4.82 | 6.03 |
| 17:30 | 3361 | Orijent Rijeka vs HNK Sibenik | 5.45 | 3.43 | 1.57 |
| 17:30 | 4069 | Telstar vs VVV Venlo | 2.23 | 3.43 | 2.82 |
| 17:30 | 4341 | Rudar Velenje vs ND Beltinci | 3.14 | 3.34 | 2.03 |
| 17:30 | 4702 | NK Dugopolje vs NK Jarun Zagreb | 1.84 | 3.43 | 3.63 |
| 17:30 | 5021 | Krizevci vs NK Belisce | 1.62 | 3.52 | 5.00 |
| 17:30 | 5072 | NK Zrinski Jurjevac vs Bsk Bijelo Brdo | 1.81 | 3.33 | 3.89 |
| 17:30 | 5772 | ND Dravinja vs NK Fuzinar Ravne | 1.99 | 3.43 | 3.18 |
| 17:30 | 5998 | FK Radnicki Sremska Mitrovica vs FK Jedinstvo UB | 2.08 | 3.03 | 3.34 |
| 18:00 | 4984 | SK Otava Katovice vs FK Spartak Sobeslav | 2.12 | 3.58 | 2.86 |
| 18:00 | 5724 | Jiskra Domazlice vs Karlovy Vary | 1.29 | 5.07 | 7.31 |
| 18:00 | 5913 | Neftekhimik vs Urozhay Krasnodar | 1.99 | 3.22 | 3.38 |
| 19:00 | 1269 | DR Congo vs Sudan | 1.70 | 3.37 | 5.09 |
| 19:00 | 2589 | Ukraine vs England | 7.12 | 4.16 | 1.47 |
| 19:00 | 3394 | Estonia vs Sweden | 7.59 | 4.64 | 1.40 |
| 19:00 | 4120 | Ivory Coast vs Lesotho | 1.15 | 6.24 | 18.72 |
| 19:00 | 5253 | Andorra vs Belarus | 4.56 | 3.13 | 1.92 |
| 19:00 | 5266 | Mauritania vs Gabon | 2.51 | 3.01 | 2.86 |
| 19:00 | 5496 | CD Cayon vs Guijuelo | 3.13 | 2.98 | 2.20 |
| 19:30 | 5451 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.24 | 2.88 | 3.38 |
| 19:45 | 3406 | Cambuur vs Den Bosch | 1.25 | 5.52 | 8.99 |
| 20:00 | 4575 | Moreirense vs Sporting Braga | 3.89 | 3.69 | 1.80 |
| 20:45 | 2113 | Cobh Ramblers vs Athlone Town | 2.36 | 3.44 | 2.53 |
| 21:45 | 1237 | Romania vs Israel | 2.01 | 3.33 | 3.81 |
| 21:45 | 2308 | North Macedonia vs Italy | 7.88 | 4.44 | 1.41 |
| 21:45 | 4393 | Kosovo vs Switzerland | 5.28 | 3.80 | 1.65 |
| 21:45 | 5830 | Germany vs Japan | 1.66 | 3.98 | 4.83 |
| 22:00 | 1699 | Leganes vs Huesca | 1.95 | 3.03 | 4.07 |
| 22:00 | 1918 | Morocco vs Liberia | 1.13 | 6.43 | 24.90 |
| 22:00 | 4349 | Senegal vs Rwanda | 1.29 | 5.08 | 9.53 |
| 22:00 | 4662 | NAC Breda vs Roda Kerkrade | 2.01 | 3.54 | 3.18 |
| 22:00 | 5538 | Comoros vs Zambia | 3.32 | 3.17 | 2.16 |
| 22:30 | 1569 | Virgin Islands, British vs Turks And Caicos Islands | 2.44 | 3.30 | 2.45 |
| 22:30 | 4642 | Antigua and Barbuda vs Guyana | 2.40 | 3.14 | 2.74 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Septemba 9, 2023

Nipashe




Neymar ajitetea kuitwa Brazil UKURASA 21



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakishangilia baada ya timu hiyo kutoka sare dhidi ya Algeria na kukata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast. **PICHA: TFF**

## Pacome kuipeleka Yanga makundi CAF

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema anaamini timu yake itatinga hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na jukumu la kufikia malengo litaongozwa na nyota wake wawili, Maxi Nzengeli na Pacome Zouzoua.

Al Merrikh ya Sudan inatarajia kuwakaribisha Yanga katika mechi ya michuano hiyo itakayochezwa Septemba 16, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema wachezaji wake wamefanya mazoezi magumu katika wiki hii ambayo yamesaidia kutambua kiwango cha kila mmoja wao huku akiamini Pacome na Nzengeli ndio wameshikilia 'moyo' wa Yanga kwa sasa.

Gamondi alisema mazoezi hayo yamewaimarisha na watarejea uwanjani wakiwa bora na kuitumikia vyema klabu yao ili kupata matokeo chanya kwenye mechi zote watakazocheza.

"Nimeona uwezo wa Maxi, Zouzoua na wengine wamefanya vizuri katika mechi zilizopita na hata mazoezini, lakini ninahitaji wawe bora zaidi kuelekea mechi ijayo dhidi ya Al Merrikh.

Kabla ya kwenda Rwanda tutakuwa na mchezo mmoja wa kirafiki ambao tutaucheza Jumamosi (leo), naamini wachezaji wangu wanaendelea vizuri na tutafikia malengo yetu," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema mechi ya kirafiki watakayocheza itamsaidia kuona maendeleo ya kikosi chake baada ya mazoezi

ENDELEA UKURASA 23

# Stars walamba mil.500 za Samia

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Awapongeza kwa kuweka tena rekodi, kocha afunguka haikuwa...

RAIS Samia Suluhu Hassan amewapongeza wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) kwa kufanikiwa kukata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazofanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwakani huko nchini Ivory Coast.

**Taifa Stars imefuzu kushiriki AFCON baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi F ikiwa na pointi nane wakati vinara wa kundi hilo Algeria ilifikisha pointi 16 baada ya timu hizo kutoka suluhu zilipokutana juzi usiku.**

Kwa mafanikio hayo, Rais Samia tayari ametekeleza ahadi yake ya kutoa kitita cha Sh. milioni 500 kwa timu hiyo, fedha ambazo tayari ziko mikononi mwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Baada ya mechi kati ya Stars dhidi ya Algeria kumalizika, Rais Samia aliipongeza timu hiyo kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuiheshimisha nchi anayoiongoza.

"Hongereni vijana wetu wa Taifa Stars kwa kufuzu michuano ya kuwania kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika 2023. Mmeandika historia, kwani hii ni mara yetu ya tatu kufuzu tangu kuanzishwa kwa mashindano haya. Nawatakia kila la kheri," aliandika, Rais Samia.

Wakati akiahirisha bunge, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa pia ameipongeza timu hiyo kutokana na mafanikio ambayo imepata.

"Ninayo furaha sana kuipongeza Taifa Stars kwa kufuzu kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika baada ya kupambana na Timu ya Taifa ya Algeria huko nchini Algeria jana (juzi).

Ninaipongeza sana timu yetu ya Taifa na kuitakia kila la heri katika mashindano yajayo. Nami nitumie fursa hii kuwasihi Watanzania wenzangu tuendelee kuwaunga mkono ili wapate hamasa zaidi na kutuletea ushindi." Majaliwa alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Saidi Yakubu, ambaye alikuwa Algeria na kikosi hicho aliwasilisha salamu za Rais Samia ndani ya vyumba vya kuvalia wachezaji, akisema tayari fedha hizo zimeshatolewa na kiongozi huyo mkuu wa Tanzania.

"Mtakumbuka wakati tukijiandaa na mechi dhidi ya Uganda kule nyumbani, mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya Sh. milioni 500 iwapo timu hii ikifuzu, nafurahi kuwaambia hizo fedha siyo tu zitatolewa, lakini zimekwishaletwa wizarani kwa ajili yenu," alisema Yakubu na kusababisha shangwe kutoka kwa wachezaji na viongozi wa Stars.

Yakubu aliwapongeza pia wachezaji kwa kusema mafanikio yote yamesababishwa na umoja na mshikamano kati ya serikali, Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), benchi la ufundi, wadau mbalimbali na soka na Watanzania kwa ujumla.

Alisema anataka kuona timu hiyo inajiandaa na kujipanga vyema kwa ajili ya kwenda kushindana katika fainali hizo za AFCON.

"Tunashukuru sana, hongereni sana kwa kazi kubwa ambAyo mmeifanya, unajua safari haikuwa rahisi, hata leo (juzi) mpaka dakika za mwisho ilikuwa bado ni mshikemshike, lakini tunawashukuru sana, mimi na wenzangu hapa tumekuja kwa niaba ya serikali, Mheshimiwa Rais, waziri na naibu wake.

Kwa pamoja na wadau wote wa serikalini, kwa maana kuongeza uwakilishi na hamasa, tumekuwa bega kwa bega na TFF katika kushirikiana wakati mwingine kuzibeba gharama za kambi pamoja malipo ya mshahara wa kocha na safari za timu hii," alisema katibu huyo.

Kocha Mkuu wa Stars, Adel Amrouche, naye aliwapongeza wachezaji wake kwa kucheza kwa nguvu, kujituma mpaka kufanikisha malengo waliyokuwa

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >